# Nipashe

Jumamosi Januari 30, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580476

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


**Gwajima** atoa maagizo mazito kuzuia ukatili wanawake, watoto

UKURASA 3



**JPM** azindua mradi wa maji uliopeleka neema kwa maelfu

UKURASA 3




UKURASA 11

## UTATA KIFO CHA DEREVA

# RC azuia mwili wake kuzikwa



• **Ni** anayedaiwa kuuawa katika purukushani na trafiki... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**VITAMBULISHO WAMACHINGA SASA KUANDALIWA KIDIGITALI**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali inatarajia kutoa vitambulisho vipya vya wamachinga vilivyoboreshwa ambavyo...

MAKALA MAALUM

**Corona ilivyopokewa kwa nidhamu ya kujifunza**

UKURASA 16




Rais Dk. John Magufuli akizindua mradi wa maji wa Ziwa Victoria kwa miji ya Kagongwa na Isaka, wenye uwezo wa kunufaisha watu 115,600. Thamani ya mradi huo ni zaidi ya Sh. bilioni 23. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**


Scan Hapa




Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play
Download on the App Store


# Waziri aagiza kuchunguzwa pango nyumba za watumishi

UKURASA 2


**MICHEZO** RATIBA VIPORO SIMBA, NAMUNGO YAANIKWA UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6

# RC azuia mwili dereva wa lori kuzikwa

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

KIFO cha dereva wa lori, Abdulrhaman Issa, aliyefariki mkoani Mbeya baada ya purukushani na askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani, kimeibua utata ambao umemlazimu Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kuingilia kati.

Katika picha za video ambazo tangu jana zilianza kuonekana kwenye mitandao ya kijamii, zinamwonyesha dereva huyo akishushwa kwa nguvu kutoka kwenye lori alilokuwa akiliendesha na askari wa Jeshi la Polisi na kumbeba 'mzega mzega'.

Askari hao wanadaiwa baada ya kumkamata dereva huyo, walimpeleka mahabusu katika Kituo cha Polisi Inyala kilichoko wilayani Mbeya kabla ya kuripotiwa kuwa amepoteza maisha akiwa katika Hospitali ya Igawilo iliyoko Uyole jijini Mbeya.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Chalamila, alisema kutokana na utata wa kifo cha dereva huyo, ameunda kamati huru ya watu wanne wasiofungamana na Jeshi la Polisi, wakiwamo madaktari kwa ajili ya kufanya uchunguzi.

Alisema mbali na kuunda kamati hiyo, pia amezuia mwili wa dereva huyo kuzikwa mpaka baada ya siku tatu kamati hiyo itakapokuwa imemaliza kazi ya uchunguzi kwa maelezo kuwa lengo ni kuhakikisha chanzo halisi cha kifo chake.

Chalamila alisema moja kati ya hadidu za rejea ambazo kamati hiyo itazitumia kwenye uchunguzi huo, ni video inayosambaa kwenye mitandao ya kijamii ikionyesha dereva huyo akitolewa kwenye gari alilokuwa anaendesha na kubebwa na askari.

Alisema taarifa alizozipata ni kwamba Januari 26, mwaka huu, dereva huyo alikuwa anaumwa na alikwenda katika Hospitali ya Chimala wilayani Mbarali kwa ajili ya kutibiwa na kwamba madaktari walishauri alazwe, lakini akaomba aendelee na safari ili akatibiwe katika Mji wa Tunduma mkoani Songwe.

Alisema madaktari walimruhusu na akaondoka kuendelea na safari yake, lakini haijulikani kama ugonjwa aliokuwa anaumwa ndiyo uliosababisha kifo chake ama purukushani zake na askari.

"Kabla ya zile purukushani, dereva huyo alikuwa anaendesha gari kwa kuyumbayumba barabarani na aliligonga gari lingine kubwa ambalo lilikuwa linaendeshwa na dereva ajulikanaye kwa jina la Raymond Mherela, ndipo askari wakamsimamisha," alisema Chalamila na kuongeza.

"Dereva huyo kwa sababu ya kushindwa kutii sheria bila shuruti kwa kushuka kwenye gari, waliamua kumshurutisha na ndiyo chanzo cha ile purukushani.

"Sasa, kuanzia hapo hatujui chanzo cha kifo chake, lakini hii kamati huru itatusaidia," Chalamila alifafanua.

Hata hivyo, kiongozi huyo wa mkoa alisema utata mwingine ulioibuka kwenye kifo cha dereva huyo ni mwili wake kuhifadhiwa katika Hospitali ya Igawilo iliyoko jijini Mbeya badala ya kupelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mbeya iliyoko katika Kata ya Inyala, jirani na tukio lilipotokea.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana, Mwenyekiti wa Chama cha Madereva wa Malori Kituo cha Tunduma, Hussein Msangi, alisema wanasubiri maelekezo kutoka kwa viongozi wa chama hicho taifa, ili watoe tamko la pamoja.

"Kwa sasa, tunaenda Inyala ambako tukio hilo lilitokea na tutaenda mpaka hospitalini ambako mwili umehifadhiwa, matamko mengine tunasubiri maelekezo ya viongozi wetu wa kitaifa walioko jijini Dar es salaam," alisema Msangi.

Nipashe ilimtafuta Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Jerome Ngowi, kuzungumzia tukio hilo lakini simu yake haikupokewa.

Baadaye jioni, msaidizi wake alipokea simu hiyo na kuiambia Nipashe kuwa alikuwa amekwenda katika Hospitali ya Chimala kufuatilia sakata hilo.




Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Daniel Malanga (kulia), akimtunuku Adinani Mvungi cheti cha kuhitimu mafunzo ya ndege nyuki 'Drone' ya wiki nne yanayotolewa na Chuo cha Usafiri wa Anga Tanzania (CATC) jijini Dar es Salaam, jumla ya wahitimu 21 wamehitimu mafunzo hayo kwa awamu ya kwanza. Katikati ni Mkuu wa Chuo cha CATC, Aristid Kanje. **PICHA: MPIGAPICHA WETU** .

# Waziri aagiza TAKUKURU kuwachunguza watumishi waliopewa nyumba za serikali

**Na James Mwanamyoto,**

MOROGORO

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, ameelekeza watumishi wa umma waliouziwa na kupangishwa nyumba za mradi wa Watumishi Housing eneo la Mkundi mkoani Morogoro, walioshindwa kulipa deni na kodi, huku wakizipangisha na kunufaika na kodi toka kwa wapangaji wao, wavunjiwe mikataba mara moja.

Vilevile, ameagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufanya uchunguzi dhidi ya watumishi hao.

Ndejembi alitoa maelekezo hayo jana kwa uongozi wa Watumishi Housing baada ya kufanya kikao na wapangaji na uongozi huo, ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliyemtaka waziri mwenye dhamana ya utumishi wa umma na utawala bora kushughulikia vikwazo vinavyoukabili mradi huo wa Watumishi Housing baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wapangaji wa nyumba hizo.

Ndejembi alifafanua kuwa, kuvunjiwa kwa mikataba ya watumishi hao kunatokana na wao kukiuka masharti ya mikataba ya ununuzi wa nyumba walizouziwa na kupangishwa na Watumishi Housing.

Aliongeza kuwa, uamuzi wa kuvunja mikataba kwa watumishi waliokiuka masharti ya mikataba, utatoa fursa kwa watumishi wengine kuzinunua na kupanga, na kuiwezesha Watumishi Housing kupata nguvu ya kiuchumi ya kujenga nyumba nyingine za gharama nafuu kwa ajili ya kuwauzia watumishi wa umma nchini.

Ndejembi aliutaka uongozi wa Watumishi Housing kutafuta mafundi haraka iwezekanavyo, ili wazikague nyumba hizo na kufanya ukarabati wa milango, madirisha, dali na miundombinu iliyopo iwapo imeharibika, ili kuwawekea mazingira mazuri ya kuishi watumishi waliozinunua na kupanga katika nyumba hizo.

Ndejembi alisema Watumishi Housing itajenga kisima cha maji chenye uwezo wa kuhifadhi maji yenye ujazo wa zaidi ya lita 10,000 kwa ajili ya kuwahudumia watumishi walionunua na kupanga nyumba hizo za Mkundi na kusisitiza kisima hicho kitakamilika ndani ya siku 14 na atahakikisha anafanya ufuatiliaji wa karibu ili ujenzi wa kisima hicho ukamilike kwa wakati.

Aliahidi kuwa ifikapo Juni mwaka huu, maji ya MOROWASA yatapatikana kwa kuwa mamlaka hiyo inajenga tangi litakalowezesha kuwahudumia watumishi walionunua na kupanga nyumba hizo zilizojengwa na Watumishi Housing.

Lengo la miradi mbalimbali ya ujenzi wa nyumba za Watumishi Housing nchini ni kujenga nyumba za bei nafuu kwa ajili ya kuwauzia watumishi wa umma, ili kuwawezesha kupata makazi bora yatakayowawezesha kuwa na nafasi nzuri ya kutoa huduma bora kwa wananchi.

HABARI KITAIFA

# Maagizo tisa ya Gwajima kukomesha ukatili kijinsia, wanawake na watoto

**Na Christina Mwakangale**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, ametoa maagizo tisa kwa maofisa ustawi wa jamii katika halmashauri nchini kuhakikisha wanatatua matatizo yaliyoko kwenye familia hasa matukio ya watu kijidhuru ikiwamo kujiua.

Tamko hilo limekuja baada ya matukio kama hayo kutokea nchini, ikiwamo la Desemba 10, mwaka jana, mkazi wa Kinondoni, jijini Dar es Salaam, akidaiwa kumkata kwa mapanga mkewe.

Dk. Gwajima aliyasema hayo jana katika tamko lake alilolitoa kwa vyombo vya habari huku akibainisha kuwa matukio hayo yamekithiri ikiwamo migogoro kuhusu mgawanyo wa mali.

Alisema tukio la Desemba 10, mkazi wa Kinondoni ambaye anadaiwa alimkata mkewe mapanga ni baada ya kumlazimisha awanyweshe sumu watoto wake ili wafe.

"Vitendo vya kikatili na kunyimwa haki havivumiliki kwenye ardhi ya Tanzania. Tusijiue, tusijidhuru au kuwadhuru wengine kwa sababu ya msongo wa mawazo wakati serikali ipo kwa ajili ya wote wanaoonewa na kunyanyaswa," alisema Dk. Gwajima.

Pia alisema tukio lingine ni kuhusu mgawanyo wa mali baada ya mama mmoja kuripotiwa kwa kutaka kujiua yeye mwenyewe na kuwaua watoto, baada ya mume wake kufariki dunia.

"Vilevile tarehe 27 Januari, katika Wilaya ya Gairo mkoani Morogoro, binti mmoja alinusurika kifo akijaribu kujiua kwa kunywa sumu, chanzo kikiwa wazazi kuingilia kuvunja uhusiano na mpenzi wake," alisema Dk. Gwajima.

Alibainisha kuwa kuwapo kwa matukio hayo ni kwamba ukatili wa kijinsia katika familia, migogoro ya mali ni matatizo ya kisaikolojia ambayo hayapaswi kufumbiwa macho na jamii.

Dk. Gwajima kwenye tamko hilo, aliwaagiza maofisa ustawi wa jamii katika kila halmashauri nchini kutenga siku moja kila wiki kusikiliza matatizo ya kijamii, kuweka daftari la kudumu la usajili na kutafuta ufumbuzi wa masuala hayo.

"Kutoa rufaa (fufani) za mapema na ufuatiliaji wa matatizo, kuweka bayana namba za simu ya maofisa ili wananchi wawapate maofisa hawa kwa njia ya simu wakati wote," alisema Dk. Gwajima.

Aliongeza kuwa maofisa hao washirikiane na serikali za mitaa katika maeneo yao, kushughulikia unyanyasaji na kuhakikisha ulinzi wa wanawake na watoto uwepo katika ngazi zote.

Dk. Gwajima alisema taarifa za matukio hayo ziandaliwe na kuwasilishwa kwa katibu tawala wa mikoa na baada ya wiki mbili ziwasilishwe kwa kamishna wa ustawi wa jamii.

Pia alitoa wito kwa wananchi ambao wanaonewa wapige simu namba 0754497122, 0739900100 kwa msaada zaidi.

## JPM azindua mradi mkubwa wa maji

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

RAIS John Magufuli amezindua mradi wa maji wa Ziwa Victoria uliopo Isaghehe utakaosambaza kata za Isaka na Kagongwa wilayani Kahama mkoani Shinyanga na kuwanufaisha watu 115,000.

Alizindua mradi huo mkubwa wa maji jana uligharimu Sh. bilioni 23.15, fedha ambazo zimetoka serikalini, huku akiwataka makandarasi wote nchini wahakikishe miradi yote inakamilika kwa wakati na kuisimamia vizuri.

Rais Magufuli alisema waliamua kutoa maji ya Ziwa Victoria kutoka jijini Mwanza hadi wilayani Kahama, ili kuwanufaisha wakazi wa Isaghehe, Kagongwa na Isaka na tayari maji yanapatikana kwenye matangi mawili yenye ujazo wa lita milioni 1.6.

"Mkoa wa Shinyanga ulipata fedha za kutekeleza miradi ya maji 24 na wameweza kuokoa kiasi cha Sh. milioni 1.5 katika utekelezaji wake, ninawataka makandarasi wote nchini kuhakikisha wanasimamia vizuri miradi ya maji, ili iwanufaishe wananchi," aliagiza.

Rais Magufuli alisema wananchi, hasa wanawake, waliteseka kutafuta maji, hivyo akaagiza matangi hayo yafunguliwe kuanzia jana ili wananchi walio karibu na maeneo hayo waanze kuchota maji kwa matumizi mbalimbali.

Kiongozi huyo alisema kuwa wakati anaingia madarakani mwaka 2015, alikuta miradi mikubwa ya maji kwa asilimia 30 haitoi maji, hivyo alisisitiza kwa awamu yake ya uongozi upatikanaji wa maji ukamilike katika vijiji vyote nchini.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema Mkoa wa Shinyanga una Sh. bilioni 52 kwa ajili ya kukamilisha miradi ya maji katika vijiji 59 na miradi 24 mikubwa ilitengewa Sh. bilioni 40 na watatumika wataalamu wa ndani.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiongoza majadiliano baada ya kufungua mkutano wa viongozi wa wamachinga kutoka mikoa yote Tanzania Bara kwenye Kituo cha Mkutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Vitambulisho vya wamachinga sasa kidigitali

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali inatarajia kutoa vitambulisho vipya vya wamachinga vilivyoboreshwa ambavyo vitakuwa na picha ya mhusika na baadhi ya kumbukumbu binafsi.

Kumbukumbu hizo zitamtambulisha na kumwezesha kupewa huduma katika maeneo mbalimbali zikiwamo taasisi za kifedha.

Amesema vitambulisho hivyo vitaanza kutolewa Aprili Mosi, mwaka huu, hivyo amewataka wakuu wa mikoa na wilaya wahakikishe wamachinga wanaendelea kufanya shughuli zao bila bugudha katika kipindi hiki ambacho muda wa matumizi ya vitambulisho vyao umekwisha.

Majaliwa aliyasema hayo juzi alipofungua mkutano na viongozi wa wamachinga kutoka mikoa yote Tanzania Bara, viongozi wa benki na baadhi ya mawaziri na watendaji wa serikali katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam.

Waziri Mkuu alisema vitambulisho hivyo vitakuwa na picha ya mhusika, hivyo haitawezekana kutumiwa na mtu mwingine na pia vitadumu kwa miaka miwili hadi mitatu tofauti na vya sasa ambavyo vilikuwa vya mwaka mmoja.

"Serikali kupitia Rais John Pombe Magufuli, imeamua kutoa vitambulisho rasmi ambavyo vitawatambulisha popote na kupata huduma muhimu kama vile kutambulika na taasisi za fedha na maeneo muhimu," alisema.

Waziri Mkuu pia aliwaagiza viongozi wa wamachinga wahakikishe wanakuwa na takwimu sahihi ya idadi ya wamachinga ili iwe rahisi kuwahudumia.

"Tuwe na kanzidata ya wamachinga ambayo itarahisisha mawasiliano ndani ya Shirikisho la Wamachinga na Serikali," alisisitiza.

Pia aliwataka wamachinga wajiunge kuanzia ngazi ya vitongoji hadi taifa ili wahudumiwe kwa urahisi.

"Mkijiunga pamoja na kutambuliwa ni rahisi kwa taasisi za kifedha kuwafikia na kuwapatia huduma za mikopo itakayowawezesha kukuza mitaji yenu," alisema.

Serikali, alisema imedhamiria kumhudumia na kumtumikia kila mwananchi wakiwamo wamachinga kwa lengo la kuwawezesha kukuza biashara zao na kujikwamua kiuchumi, hivyo aliwataka wafanye kazi kwa bidii.

HABARI KITAIFA

## RIPOTI MAALUM -2

# Wanyama hawa marufuku kwenye bucha nyamapori

**SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA), ilibainisha wanyamapori ambao nyama yao ni marufuku kuuzwa kwenye bucha za nyamapori nchini. Endelea na sehemu ya pili ya ripoti hii kujua mustakabali wake**

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

NAIBU Kamishna wa Utalii, Huduma za Biashara na Utalii wa TAWA, Imani Nkuwi, alifafanua kuhusu uanzishwaji wa bucha za wanyamapori hizo akisema:

"Ninadhani labda tutaeleweshana, mnatafuta nini na kwa nini, labda ukienda utatumia siku saba, nane, tisa hadi 10. Kwenye uwindaji wa kitalii tunazo 'packages' za 'five star'.

"Tuna permit (vibali) vya siku 10, yaani ukiomba package (mgao) wa wanyama fulani, tutakupa package ya siku 10 na utalipa siku 10. Kuna wanyama ukiomba package ya siku 14 tutakupa na utalipa siku 14. Kuna wanyama ukiomba kuna package ya siku 21 na utalipa siku 21."

Alisema vyanzo ambavyo vinahusisha uwindaji, ambavyo wengi waliamua kuvichagua, vina utafutaji, akibainisha kuwa wapo watu hutokea kwenye kutafuta, wanakata tamaa na kurudi nyumbani.

Nkuwi, alisema ili kumaliza ombwe hilo, TAWA imeamua kuwatumia miongoni mwa wadau wenye uzoefu wa miaka 35 na kuendelea katika tasnia ya uwindaji kutoa mafunzo kwa wenye bucha za nyamapori.

### MGAO KITAIFA WAJA

Kwa mujibu wa Naibu Kamishna Nkuwi, maeneo yanayotumika kwa uwindaji wa kitalii, uwe uwindaji wa wakazi na wenyeji, ni lazima kuwe na mgao.

Mgao huo kwa sasa unafanyika kisayansi na unafanywa na kamati ya wanazuoni inayoongozwa na Mwenyekiti wake Dk. Rosemary kutoka Taasisi ya Utafiti wa Wanayampori Njiro, Arusha.

"Wanakuja na idadi ambayo ukiiondoa katika ile ecosystem (mwingiliano wa wanyama), haitaathiri uendelevu wa wale wanyama wetu katika kizazi hiki na kizazi kijacho. Wanatutengenezea kitu kinaitwa 'National Quoter' au mgao wa taifa wa kuwinda wanyama.

"Huo mgao wa taifa wa kuwinda wanyama kwa miaka mitatu kumekuwa na wanyama, ukichanganya na aina za ndege wachache wanaowindwa wanafikia 42,000. Hao ndio wanyama ambao unaweza ukawatoa wakatumika kwa shughuli mbalimbali, ambao ni wanyama wanaowindwa kwa Tanzania au wawe ni wanyama wanaowindwa na watalii.

"Iliposemwa bucha, watu wakatengeneza picha, hizo bucha zitakuwa kama bucha za nyama zilivyo."

"Upatikanaji wa malighafi ya kudumu itatokana na ufugaji wa wanyamapori."

Alisema kuwa katika eneo hilo la ufugaji, tangu wameanza kuhamasisha, kulikuwa na mashamba na ranchi za wanyamapori 21, lakini kwa sasa ziko 61.

"Mwezi ujao (Februari), nimeona tangazo la ofisi yangu, linatangaza watu ambao wanahitaji kuomba leseni za kufuga wanyamapori kwa ajili ya robo, inayoishia Desemba na inayoanza mwezi Aprili.

"Kwa hiyo, tutakuwa na kazi ya kutoa leseni kwa Watanzania wanaopenda kufuga wanyamapori, ili hii tasnia mpya au biashara mpya ya bucha za wanyamapori iwe endelevu," alisema.

### MAELEKEZO YA JPM

Akifafanua zaidi katika mkutano huo, Naibu Kamishna Nkuwi, alisema kwamba ukifuatilia vizuri, maagizo mawili ya Rais John Magufuli aliyoyatoa akiwa Chato mkoani Geita wakati wa uzinduzi wa Hifadhi ya Taifa ya Burigi/Chato, aliwahamasisha Watanzania kufuga wanyamapori, ndiyo chimbuko la bucha hizo.

Pili, aliwapa maelekezo wizara, kupunguza bei ya wanyama wa mbegu na akawapa maelekezo mengine, kwa sababu walikuwa wanatoa leseni za ufugaji mara moja kwa mwaka, lakini kwa sasa wanatoa leseni mara nne kwa mwaka.

"Ukiangalia lengo lake kubwa lilikuwa ni kuhamasisha Watanzania wengi waingie kwenye ufugaji wa wanyamapori. Halafu baadaye akatoa agizo kwamba sasa Watanzania wafungue biashara ya bucha za wanyamapori ili Watanzania wengi wapate kitoweo.

"Kwa hiyo, ukiyaangalia maagizo haya mawili yanakuonyesha maono, kwamba ili uweze kuwa na biashara ya bucha ambayo ni endelevu na haitakuwa tegemezi kwenye uwindaji maeneo ya asili, kuna kitu kinaitwa mgao wa mwaka.

"Kwa hiyo yale mategemeo kwamba tunaweza kuwa na bucha za nyamapori kama zilivyo bucha za ng'ombe, kwa kutegemea mgao wa wanyama 42,000 tunawatoa kwa mwaka, haiwezi kuwiana na upatikanaji wa nyama za wafugaji wa ng'ombe 350,000 wanaoliwa nchini kwa mwezi. Huku kwenye wanyamapori ni 42,000 kwa mwaka.

### HAWAJAKURUPUKA

Alisema wanasisitiza kuwapo kwa mashamba hayo kwa kuwa matumizi ya mashamba ya wanyamapori ni muhimu zaidi, badala ya kutegemea maeneo ya uwindaji wa asili, kwa kuwa tija yake imeonekana katika nchi za Bostwana, Afrika ya Kusini na Zimbabwe.

"Zile nyama zinazouzwa Bostwana, Afrika ya Kusini na Zimbabwe, zile nyama zinazouzwa kule nyingi zinatoka kwenye ranchi na mashamba ya wanyamapori wanaofugwa," alisema.

### WADAU WAFUNGUKA

Akizungumza katika mkutano huo, mratibu wa wadau wa bucha za nyamapori nchini, Emanuel Absalom, alisema tangu Desemba mwaka jana, Watanzania walikuwa wameshafungua bucha hizo.

"Tunamshukuru Mheshimiwa Rais John Magufuli kwa fursa hiyo ambayo ametupatia sisi Watanzania kufungua bucha za wanyamapori.

"Tumepokea kwa furaha na imeongeza ajira na kipato kwa sisi Watanzania.Tunawashukuru TAWA katika kufungua hizo bucha na sasa tunatambulika rasmi katika mamlaka husika.

"Ni kweli tumefungua bucha na mpaka sasa hatujafikia ufanisi wa kiutendaji kwa sababu ya matatizo madogo madogo, mojawapo ni upatikanaji wa hawa wanyama, kwa sababu maeneo machache ambayo yalikuwa yametengwa kwa majaribio," alisema.

Absalom ambaye ni katibu wa wadau wa bucha za nyamapori kwa mikoa ya Kanda ya Kaskazini ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga, alisema mpaka sasa TAWA imetoa maeneo 10 ya kikanda kwa ajili ya majaribio ya uwindaji wa kawaida.

Licha ya majaribio hayo, mratibu huyo alisema wanaishukuru serikali kuliona jambo hilo na kuwaita kuwapa semina ambayo itawapa mwelekeo mpya na mtazamo mpya wa namna watakavyofanya biashara hiyo na kujadiliana vikwazo na kuvitatua kwa pamoja.

"Uwekezaji wa sasa wa mashamba ya wanyamapori, hayo ndiyo tunaona ndio dira kuu itakayokuwa ni chanzo kikubwa cha kufanya bucha zetu ziendelee kupata nyama, baada ya kuwa tumefuga wanyama hawa, hata kama litachukua muda," alisisitiza.

# Serikali kushirikiana na NGO

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema itaendelea kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO), ili kuharakisha utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa wananchi.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam katika mkutano na kikao kazi kati ya serikali na mashirika hayo.

Alisema serikali inatambua mchango wa mashirika hayo nchini katika kuleta maendeleo huku akiyahakikishia kuyapa ushirikiano.

"Serikali inatambua mchango wa NGO, hivyo niwahakikishie serikali ipo tayari kuendelea kushirikiana nanyi," alisema Dk. Mollel.

Kadhalika, Dk. Mollel aliwataka viongozi walioko katika ngazi za mikoa nchini kubainisha shughuli zinazofanywa na mashirika hayo, ili kuyatambua na kuongeza uwajibikaji.

Katibu Mkuu wa Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo Yakiserikali (NaCoNGO), Focus Magwesela, alisema hadi Januari 17 mwaka huu, jumla ya NGO 11,089 zilikuwa zimesajiliwa.

Magwesela alisema kati ya mashirika hayo, 326 ni ya kimataifa na ya ndani 8,622, huku 672 yakisajiliwa kwenye mikoa na ngazi ya wilaya ni 1,099.

"NGO tunapendekeza vibali vihamishiwe kwa maofisa kutoka ofisi za ustawi badala ya kuwa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Kwa kuwa wakati mwingine vibali vinakwamisha utendaji kazi wa mashirika," alisema Magwesela.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Foundation for Civil Society (FCS), Francis Kiwanga, alisema kikao hicho kimetoa njia na mwongozo katika kuboresha utendaji kazi na majukumu wa mashirika hayo.

"Tumekubaliana na serikali kuwa na mkutano kila mwaka, ili kupitia kanuni ambazo hazitekelezeki, hazizingatiwi na kubadilishwa."

Alisema matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa mashirika hayo pamoja na serikali yakiboreshwa, yatasaidia mashirika hayo kutochukua muda mwingi kusafiri umbali mrefu ili kuandaa taarifa za utendaji kazi na kuwasilisha serikalini.



Abiria wakipita madirishani kwenye kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho jijini Dar es Salaam, jana, ili kuwahi kupata sehemu ya kukaa, kutokana na shida ya usafiri. **PICHA: SABATO KASIKA**

## 'Jitokezeni kuwasaidia watoto wa kike shuleni'

**Na Sabato Kasika**

OFISA Elimu Mkoa wa Dar es Salaam, amewaomba wadau wa elimu, kuunga mkono juhudi za kuwawezesha wanafunzi kupata taulo za kike, ili wahudhurie shuleni kikamilifu.

Abdul Maulid aliyasema hayo jana alipopokea taulo hizo zilizotolewa kwa ajili ya wanafunzi 1,000 na Taasisi ya Flaviana Matata.

Alisema wadau wengine wanatakiwa kuunga mkono kile ambacho kimefanywa na taasisi hiyo, ili kuwapunguzia watoto wa kike tatizo hilo ambalo linasababisha wakose masomo kwa muda wa wiki moja.

"Taulo za kike ni muhimu kwa maudhurio yao ili kuwawezesha kusoma kikamilifu na kupata haki misingi ya elimu sawa na vijana wa kiume, hivyo wadau wote waunge mkono juhudi hizi," alisema Maulid.

Alisema ushirikiano wa mashirika ya umma, watu binafsi na taasisi kama ya Flaviana Matata, unahitajika kufanikisha afya ya hedhi shuleni na kuwezesha wasichana kupata haki ya elimu.

Mwanzilishi wa taasisi hiyo, Flaviana Matata, alisema ufadhili huo wa taulo kwa wanafunzi 1,000 ni wa mwaka mmoja na utagharimu Sh. milioni 54.

"Ufadhili huu umepatikana baada ya kuchangia fedha kupitia kampeni ya Donate A Period iliyofanywa na mimi pamoja na baadhi ya marafiki zangu nchini Marekani kwa lengo la kuhakikisha watoto wa kike hawakosi masomo kwa sababu ya kutomudu gharama za taulo za kike," alisema Flaviana.

Alisema kati ya wanafunzi 1,000 watakaofaidika na taulo hizo, 250 ni wa shule za Mkoa wa Dar es Salaam na wengine wa shule za mikoa mbalimbali zikiwamo za msingi na sekondari.

"Ninafurahi tumeweza kufanikisha huu ufadhili kwa mabinti 1,000 ambao kwa namna moja ama nyingine, utaenda kubadilisha maisha yao, hasa wakiwa shuleni na ninatamani ufadhili huu uwe mwanzo wa kuhamasisha serikali, kampuni binafsi na jamii kwa ujumla kuunga mkono juhudi hizi," alisema.

# Maofisa kilimo wapewa jukumu uhaba wa mafuta

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

KATIBU Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, amewataka maofisa kilimo na wadau wa ugani kuweka mikakati ya kuliondoa taifa katika utegemezi wa kuagiza nje bidhaa zitokanazo na mazao ya kilimo, ili kuipunguzia serikali mzigo wa kutumia kiasi kikubwa cha fedha kila mwaka.

Kusaya aliyasema hayo jana jijini Dodoma alipofungua kikao kazi cha Wizara ya Kilimo, maofisa kilimo na wadau wa huduma za ugani nchini.

Alisema taifa limekuwa likitumia kiasi kikubwa cha fedha katika kuagiza bidhaa mbalimbali nje ya nchi.

Kusaya alisema maofisa kilimo pamoja na wadau wa ugani nchini wanatakiwa kuhakikisha inakuwapo mikakati ya kuliondoa taifa katika utegemezi wa bidhaa mbalimbali zitokanazo na mazao ya kilimo.

"Hivi sasa taifa limekuwa na utegemezi mkubwa wa bidhaa mbalimbali zitokanazo na mazao ya kilimo kama vile ngano, mafuta ya kula na sukari.

Katibu Mkuu huyo alisema kutokana na utegemezi huo, taifa limekuwa likitumia kiasi cha Sh. bilioni 470 kila mwaka kwa ajili ya kuagiza mafuta ya kula nje ya nchi.

"Pia serikali imekuwa ikitumia kiasi cha Sh. bilioni 1.03 kila mwaka kwa ajili ya kuagiza unga wa ngano nje ya nchi kiasi ambacho ni mzigo mkubwa kwa taifa," alisema Kusaya.

Alisema kutokana na hali hiyo, maofisa kilimo wanatakiwa kuwasaidia wakulima kulima kibiashara, ili kukuza uchumi wao na taifa kwa ujumla.

Alibainisha kuwa ili taifa lipige hatua kiuchumi, sekta ya kilimo inatakiwa kufanya mabadiliko makubwa na kuacha kufanya kazi kwa mazoea.

"Tukiweka tija kwenye kilimo, tutapiga hatua katika kuondokana na vikwazo vya utegemezi kwa bidhaa zitokanazo na mazao ya kilimo.

"Hivi sasa taifa linakabiliwa na upungufu wa tani 60,000 za sukari, lakini kama tungekuwa tumejipanga vizuri kupitia wataalamu wetu, hali hii isingekuwapo.

"Ukiangalia taifa kama Israel, wana eneo dogo la kilimo, lakini wanazalisha kwa tija. Hii ni kutokana na uwekezaji mkubwa walioufanya katika setka hiyo na kutumia mifumo ya kiteknolojia ya kisasa," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Charles Mwijage, alisema kama serikali haitafanya uwekezaji mkubwa katika sekta ya kilimo, uchumi wa viwanda itakuwa ni ndoto.

Mwijage alisema kutokana na sekta za kilimo na mifugo kuwajumuisha watu wengi, kuna kila sababu uwekezaji wake kuwa kama ilivyo kwenye miradi mikubwa ya kimkakati.

"Sekta hizi za uzalishaji zikisimamiwa kwa kiwango cha juu katika taifa letu, tutapiga hatua kubwa kiuchumi na kuondokana na umaskini," alisema Mwijage.




Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigela (katikati), akikagua mradi wa kilimo cha umwagiliaji ulioko Kata ya Mombo, wilayani Korogwe, jana. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Serikali yachukua hatua majanga kazini

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema inachukua hatua za makusudi kulinda nguvu kazi yake dhidi ya majanga, ajali na magonjwa yatokanayo na kazi yanayoweza kutokea na kuwaathiri wafanyakazi hususan katika kipindi ambacho nchi inajenga uchumi imara wa viwanda.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Watu Wenye Ulemavu), Ummy Nderianaga, aliyasema hayo jana alipofunga mafunzo ya usalama na afya kazini yaliyotolewa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) kwa watumishi wa Shirika la Umeme (TANESCO) mkoani Mwanza.

Nderiananga alisema TANESCO ina nafasi muhimu katika kuliwezesha taifa kufikia agenda yake ya kujenga uchumi wa viwanda, akisisitiza ufanisi wa shirika hilo unategemea uwapo wa wafanyakazi ambao watakuwa salama na wenye afya njema.

"Bila shaka mnatambua umuhimu wenu na shirika lenu katika kufanikisha agenda ya nchi yetu ya kuimarisha uchumi kupitia mageuzi ya viwanda. Ili kufikia azma hiyo, ni lazima kuwe na umeme wa uhakika.

"Hata hivyo, upatikanaji wa uhakika wa nishati hiyo muhimu unategemea uwapo wa watumishi wenye afya njema na wenye ujuzi stahiki kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao," alisema.

Naibu waziri huyo aliongeza kuwa ili jitihada zinazochukuliwa na serikali katika kuleta maendeleo hususan ujenzi wa miradi mikubwa ya umeme na miradi mingine ziwe na tija, ni lazima kuhakikisha nguvu kazi yake inalindwa ipasavyo.

"Kutokana na sababu hii ya msingi, ndiyo maana leo mpo hapa ili kupewa nyenzo za kujiepusha na madhara ya ajali na magonjwa yanayoweza kujitokeza katika maeneo yenu ya kazi.

"Kwa sababu hiyo, ninaupongeza uongozi wa shirika pamoja na OSHA kwa kuliona hilo na kuchukua hatua kwa wakati," alisifu.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema mafunzo hayo yaliyojikita katika masuala ya utoaji wa huduma ya kwanza mahali pa kazi, yaliyotolewa kwa takribani siku tisa kwa makundi matatu tofauti ya watumishi wa TANESCO, kila kundi likipata mafunzo hayo kwa siku tatu.

Alisema zaidi ya watumishi 120 wa TANESCO kutoka katika mikoa mbalimbali, wamepatiwa mafunzo ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao katika hali ya usalama na afya.

"Tunafahamu TANESCO mnafanya kazi ambazo ni hatarishi, hivyo pamoja na kwamba mna fahamu, tumeona kuna umuhimu wa kuendelea kukumbushana, ili kuokoa maisha au kupunguza madhara pale ajali au magonjwa yanapotokea katika sehemu zetu za kazi," alifafanua.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Dk. Phillis Nyimbi, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, katika hafla hiyo, alisema OSHA imekuwa ikifanya vizuri katika Kanda ya Ziwa hususan katika kutoa miongozo na maelekezo kuhusu masuala ya usalama na afya mahali pa kazi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Taifa Stars imulikwe upya ilipoangukia CHAN 2021

**KWA** mara nyingine tena safari ya timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, kwenye Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zinazoendelea nchini Cameroon, imeishia hatua ya makundi kama ilivyokuwa mwaka 2009 nchini Ivory Coast.

Katika fainali za 2009, Tanzania ambayo ilipangwa Kundi A na Senegal, Zambia pamoja na wenyeji Ivory Coast, ilimaliza hatua ya makundi ikishika nafasi ya tatu ikiwa na pointi nne kama ilivyokuwa mwaka huu katika fainali hizo ikiwa Kundi D.

Kwenye kundi hilo mwaka 2009, Zambia iliongoza kutokana na tofauti nzuri ya mabao ya kufunga na kufungwa, ikiwa na pointi tano sawa na Senegal ambazo zilitinga hatua ya robo fainali huku Tanzania na Ivory Coast iliyoburuza mkia katika kundi hilo ikiwa na pointi moja zikiaga mashindano hayo yaliyoanza kufanyika kwa mara ya kwanza mwaka huo.

Hata hivyo, wakati Watanzania wengi wakiwa na matumaini makubwa kuwa pengine, baada ya kuzikosa fainali hizo kwa kipindi cha miaka 10, Taifa Stars ingeweza kufanya makubwa mwaka huu, hali hiyo imejirudia tena kama ilivyokuwa 2009.

Ni matokeo ambayo yanafanana, kwani mwaka 2009, Taifa Stars ilianza kwa kupoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Senegal kisha ikashinda 1-0 dhidi ya Ivory Coast kabla ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Zambia, mchezo ambao ilitakiwa kushinda ili kutinga robo fainali.

Kwa mwaka huu nchini Cameroon, Stars ilianza kwa kupoteza kwa mabao 2-0 dhidi ya Zambia kisha ikashinda bao 1-0 dhidi ya Namibia kabla ya kutoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Guinea, hivyo kuwashuhudia Waguinea hao na Wazambia wakitinga robo fainali na Tanzania na Wanamibia wakirejea nyumbani.

Hapa kuna somo kubwa kwa Taifa Stars kujifunza katika mashindano haya yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF) na mengine ya kimataifa ambayo mara nyingi hujumuisha timu nne katika kila kundi.

Kwa namna ambavyo Nipashe limekuwa makini kufuatilia hatua kwa hatua katika mashindano yote Taifa Stars imekuwa ikishiriki, limegundua udhaifu mkubwa wa kukubali kuanza kinyonge, ambao hufanywa na wachezaji pamoja na benchi la ufundi la kikosi hicho.


Ukichunguza mara nyingi Taifa Stars katika mechi zake ziwe za kuwania kufuzu michuano mbalimbali ama mashindano, huanza kwa kukubali kipigo ama kuambulia sare, jambo ambalo huigharimu timu hiyo pindi inapozinduka wakati huo wapinzani wao wenyewe hawakihitaji sare ama ushindi ili kusonga mbele.

Tunahitaji kuiona Taifa Stars sasa ikiandaliwa kuanza mashindano yoyote kwa kucheza mechi ya kwanza kama fainali kwa wachezaji kuhamasika na kucheza kwa ari kama ambavyo imekuwa ikicheza mechi zake za mwisho ambazo huamua hatima yake. Tunaamini kama Stars ingecheza mechi ya kwanza kwa ari, hamasa na kiwango cha juu kama ambavyo ilicheza dhidi ya Guinea mwaka huu, ama ilipohitimisha mchezo wa mwisho dhidi ya Zambia fainali za 2009, ni dhahiri ingetinga robo fainali na hata kufika fainali.

Hivyo, tunachotarajia kukiona kwa sasa si kuanza kunyosheana vidole kwa makosa yaliyofanyika, bali kuanzia sasa ni Shirikisho la Soka nchini (TFF), benchi la ufundi la Stars chini ya Kocha Mkuu, Etienne Ndayiragije, kutazama ni wapi timu hiyo inapojikwaa kwa kufanyika maandalizi ya kina, huku umakini katika uteuzi wa wachezaji watakaounda kikosi hicho ukimulikwa zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Kwa hili la Bumbuli, TFF kuna inapokosea

**WIKI** hii, Kamati ya Maadili ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), pamoja na mambo mengine, ilimfungia Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, kujihusisha na shughuli zote za soka ndani na nje ya nchi kwa kipindi cha miaka mitatu.

Bumbuli alifungiwa kwa kile kilichoelezwa ni kutotii uamuzi wa kamati hiyo uliotolewa Septemba mwaka jana wa kutakiwa kulipa faini ya shilingi milioni tano.

Hii ilitokana na kauli alizozitoa wakati kesi ya mchezaji Bernard Morrison ikiendelea dhidi ya Yanga, huku wenzake aliohukumiwa nao, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Klabu ya Simba, Haji Manara na Mjumbe wa Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya TFF, Zacharia HansPope wakilipa faini zao siku chache baada ya hukumu.

Hata hivyo, kwenye mitandao ya kijamii zinasambaa picha zinazoonyesha risiti ya benki moja nchini, ilionyesha kuwa Bumbuli alilipa faini hiyo Januari 22, mwaka huu na imeingia kwenye akaunti ya TFF.

Na mkakanganyiko unajitokeza zaidi kwani inadaiwa kuwa hakuna sehemu yoyote inayoonyesha kuwa faini hiyo ilitakiwa ilipwe lini.

Je, Bumbuli alilipa faini hiyo wakati wajumbe wa kamati hiyo wakiwa bado hawajaangalia akaunti ya TFF kuona kama kuna pesa imeingia au la?

Au wajumbe wa kamati walifanya yao kwa sababu waliona Bumbuli alichelewa kulipa fainali hiyo? Je, kuna tarehe ya mwisho wa kulipa iliyowekwa? Hapo ndipo utata uliko.

Wapo wanaosema kama ni hivyo, basi pesa zirudishwe na adhabu iendelee. Hawaoni sababu ya TFF kuchukua pesa hizo za faini wakati tayari mtuhumiwa ameshahukumiwa kwa kufungiwa.

Kama hakukuwa na mwisho wa tarehe ya kulipwa pesa hizo, basi haiwezekani faini ilipwe halafu mtuhumiwa afungiwe pia. Kimoja kati ya hicho ndicho kinatakiwa kifanyike.

Ukiliangalia sana suala hili utaona kuwa kinachotakiwa kifanyike sasa ni mazungumzo ya pande zote. Kamati ya Maadili ya TFF na Yanga, pamoja na Bumbuli mwenyewe ili kuona namna ya kuyamaliza.

Kama Bumbuli angekuwa hajalipa faini hiyo sawa, lakini kwa sababu imelipwa, hata kama imechelewa, lakini busara ingetumika zaidi kwa ama kwa kupigwa penalti kwa kutokana na kuchelewa kulipwa, kwa sababu wote ni wanafamilia ya soka na si kumpa adhabu kali kama hiyo ya kumfungia kwa kipindi cha miaka mitatu.

Pia kamati inabidi iangalie na kupitia upya kanuni zake kwani kwa dunia ya soka la sasa hakuna kufungiana miaka mitatu kama zamani, kama kosa lenyewe si la rushwa au kupanga matokeo.

Kanuni za kufungiana ni za kizamani kwa sababu enzi hizo mpira ni ridhaa, kwani mwenyekiti wa klabu, makamu mwenyekiti, katibu, katibu mwenezi, mweka hazina, wote walikuwa wanafanya kazi kwa kujitolea, kila mmoja akiwa ameajiriwa kwenye shirika, kampuni, au amejiajiri yeye binafsi.

Hapo hata mtu akifungiwa miaka mwaka mmoja au mitatu, anaendelea na maisha yake kama kawaida, lakini tangu Tanzania ilipoingia kwenye soka la kulipwa na watendaji wake baadhi kuwa wa kuajiriwa, mambo ya kufungiana yamepitwa na wakati na badala yake faini tu ndizo zinatawala.

Mfano Makatibu Wakuu, Maofisa Watendaji Wakuu na Maofisa Habari wa Klabu kwa sasa wote ni waajiriwa na wanalipwa mshahara na klabu zao, haiwezekani kuwafungia kwa sababu hiyo ndiyo ajira yao inayowafanya waishi na familia zao.

Shirikisho la Soka Duniani (FIFA) imelifanya soka kama sekta rasmi ya ajira duniani kote, ndiyo maana siku hizi huwezi kusikia mchezaji anafungiwa miezi mitatu, sita au mwaka kama zamani kwa kesi za kimkataba au hata za kikanuni za uwanjani.

Ukiona mchezaji kafungiwa muda huo, basi ameunajisi mchezo wa soka kwa kujiingiza kwenye kubeti, rushwa au kupanga matokeo.

Mfano tangu mwanzo wakati Bumbuli anaonekana kukaidi kulipa, kamati ingeiagiza TFF kuikata Yanga kwenye baadhi ya mechi zake kwa ajili ya kulipa faini hiyo na Yanga kumkata mwajiriwa wao kupitia mshahara wake na si kwa hiki ambacho kimefanyika.

# Kampuni zaomba kununua na kuchakata gesi asilia TPDC

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), limesema limepokea maombi ya kampuni mbalimbali zinazotaka kununua gesi asilia na kuibadilisha kuwa kimiminika na kuisafirisha kwenye mikoa ambayo haina nishati hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dk. James Mataragio, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam mbele ya Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati, Stephen Byabato, ambaye alifanya ziara katika maeneo matatu ya kuzalisha umeme, kuupooza na kuusafirisha.

Baada ya Naibu Waziri kufika katika kituo cha kuzalisha gesi asilia Kinyerezi, alitaka kujua TPDC imejipangaje kuiuza baada ya mradi wa umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere utapoanza na matumizi ya gesi kupunguza katika gridi ya taifa.

Dk. Mataragio alimweleza Byabato kuwa mpaka sasa ziko kampuni ambazo zimeomba kununua gesi ili kuibadilisha kuwa kimiminika na kuiuza katika maeneo yasiyo na mabomba kama Tanga, Mwanza na Mbeya.

"Baada ya uzalishaji umeme Bwawa la Mwalimu Nyerere kukamilika, matumizi ya gesi yatapungua. Kwa sasa matumizi ya gesi inayopita katika gridi ya taifa asilimia 60 inatokana na gesi asilia inayotoka hapa Kinyerezi," alisema.

Alisema kwa sasa wanazalisha futi za ujazo milioni 200 ambazo baadhi zinakwenda viwandani, kwenye makazi na gridi ya taifa.

Kuhusu kiwanda cha mbolea cha Mtwara ambacho kiliomba kipatiwe gesi futi za ujazo milioni 100 kwa siku, Dk. Mataragio alisema walishindwa kufanya hivyo kwa sababu kwa siku kituo hicho kinazalisha futi za ujazo milioni 200 hivyo wangezitoa maana yake nchi ingekosa umeme.

"Matarajio yetu ujio wa Bwawa la Mwalimu Nyerere utasaidia matumizi ya gesi inayozalishwa iende kwenye kujenga viwanda kwa kusambazwa katika matumizi mengine," alisema.

Alitaja baadhi ya viwanda vilivyoomba gesi kuwa ni pamoja na vile vinavyozalisha mbolea na hivyo vinavyoibadilisha nishati hiyo kuwa kimiminika.

Pia alisema kwa mwaka huu katika historia ya nchi, wamefanikiwa kuzalisha gesi nyingi zaidi inayofikia futi za ujazo milioni 211. Pia alisema hiyo inaonyesha matumizi ya gesi yanaongezeka siku hadi siku.

Akizungumza na waandishi wa habari, Byabato alisema amekwenda kituo cha kupooza umeme kilichoko Kigamboni ambacho kimefikia asilimia 92 za ukamilishaji na baadaye alitembelea Kinyerezi II kujionea shughuli zinazoendelea pale.




Ofisa Elimu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abdul Maulidi (kulia), akipokea boksi lenye taulo za kike jana, kutoka kwa mwanzilishi wa Taasisi ya Flaviana Matata Foundation, Flaviana Matata, katika uzinduzi wa ufadhili wa taulo hizo kwa wanafunzi 1,000 unaofanywa na taasisi hiyo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wazazi waonywa kutopeleka watoto shuleni

**Na Julieth Mkireri,** MKURANGA

MKUU wa Wilaya ya Mkuranga, Filberto Sanga, amewataka madiwani wa halmashauri hiyo kuwahamasisha wazazi na walezi kuwapeleka watoto shuleni kabla hawajachukuliwa hatua za kisheria.

Sanga alitoa agizo hilo juzi wakati wa hafla fupi ya kuwakabidhi wakuu wa shule za sekondari madawati 1,000, ili kuondoa uhaba wa samani shuleni sambamba na kutekeleza agizo la Waziri Mkuu Kassim Majaliwa la kutaka wanafunzi wawe wamekaa kwenye madawati ifikapo Februari 28, mwaka huu.

Mkuu huyo wa Wilaya alisema hakuna sababu ya kuwafanya wanafunzi wanaostahili kuwa shuleni kuendelea kubaki nyumbani ilihali vikwazo katika sekta ya elimu vinatatuliwa na serikali.

Alisema ni vyema kila diwani katika eneo lake akasimamia suala hilo, ili wanafunzi wapate haki yao ya msingi na wazazi ambao wataonekana kuwa kikwazo taarifa zao zitolewe ili wachukuliwe hatua.

Akikabidhi madawati hayo, Sanga aliwaomba wadau wa maendeleo ndani na nje ya mkoa wa Pwani kuendelea kusaidia harakati za kukabiliana na ukosefu wa madawati linaochangiwa na ongezeko la wakazi wanaohamia na watoto kutoka maeneo tofauti kutokana na uwapo wa viwanda vingi katika wilaya. Katika hatua nyingine, Sanga aliwapongeza madiwani na waatalamu walio chini ya ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya, Mhandisi Mshamu Munde, kwa kutoa Sh. milioni 533 walizozielekeza katika ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari

Alimshukuru pia Rais John Magufuli kuwachangia Sh. milioni saba na Mbunge wa Mkuranga, Abdalla Ulega, aliyechangia Sh. milioni mbili.

# Madiwani wang'aka huduma mbovu afya

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, wamelalamikia ubovu wa huduma zinazotolewa katika Hospitali ya Wilaya hiyo na kumtaka Mkurugenzi Mtendaji kukaa na wataalamu kuweka mikakati ya kuokoa maisha wa wananchi.

Malalamiko hayo yalitolewa na Diwani wa Viti Maalumu Tarafa ya Matemanga, Stawa Timamu, wakati akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika juzi.

Alisema hali hiyo imekuwa kikwazo kwa wananchi kwenda kupata huduma hospitalini hapo na kwamba endapo wataalamu hawatadhibitiwa iko hatari ya kutoa mwanya kwa wananchi kuanza kwenda kutibiwa kwa waganga wa kienyeji.

Diwani Timamu alisema kumekuwa na malalamiko mengi ya ubovu wa huduma kutoka kwa wagonjwa na wauguzi wanaokwenda kupata huduma katika hospitali hiyo.

Timamu alizitaja baadhi ya kero zinazowakabili wagonjwa ni pamoja na kutopatiwa huduma yoyote bila kutoa rushwa, matumizi ya lugha za matusi, hospitali kutokuwa na dawa na ikitokea wameenda kununua dawa nje, wakati mwingine huwa hazitumiwi na wagonjwa wao.

Alisema pia ziko taarifa pia wananchi wamekuwa wakilalamikia kutozwa fedha kwa makundi ya wanawake wanaokwenda kujifungua, ambapo vifaa vyote hununuliwa na walengwa na endapo atafika hana fedha za kununulia, hawapatiwi huduma.

Hali hiyo, alisema imekuwa ikisababisha vifo vingi kwa wanawake na watoto ambavyo hutokana na kukaa muda mrefu wakiwa wanasukuma bila kupatiwa usaidizi.

Alisema makundi mengine ambayo hutozwa fedha ndipo watibiwe ni pamoja na wazee na watoto chini ya miaka mitano ambao serikali imeelekeza kupatiwa huduma za matibabu bure na kwamba ikitokea mgonjwa ameenda huku ndugu wakiwa hawana fedha anaweza kupoteza maisha kwa kutopata huduma.

## Jamii yashauriwa kupata msaada wa kisheria bure

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JAMII imetakiwa kutumia kituo cha msaada wa kisheria cha Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa vitendo, ili kupata msaada huo bure kwenye masuala mbalimbali ikiwamo mirathi.

Ofisi Habari Elimu na Mawasiliano kutoka Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, Scholastica Njozi, alitoa wito huo jana katika maonyesho ya Wiki ya Sheria na maadhimisho ya miaka 100 ya mahakama, yanayofanyika jijini hapo.

Alisema taasisi hiyo imeanzisha kituo hicho Februari, mwaka jana na kutoa msaada kwa Watanzania zaidi ya 140 waliokuwa hawana uwezo wa kulipa gharama za mawakili.

"Lengo kuu la taasisi yetu kuweka kituo hichi kutoa msaada bure kwa kuwa inatoa mafunzo kwa vitendo na tuliona ni bora wanafunzi wetu kupata eneo la kutoa msaada wa kisheria kwa jamii kwa kile wanachosoma, pia kutoa huduma kwa Watanzania ambao wengine hawana uwezo wa kulipa gharama za Mawakili," alisema.

Alisema wanatumia wanafunzi na walimu kwa kushirikiana na Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), kwa kesi ambazo zinahitaji uwakilishi mahakamani.

"Tunashirikiana na TLS kusimamia kesi za watanzania ambao hawana fedha za kulipa mawakili, na tunawajengea hali ya kujitoa kwa ajili ya Watanzania ambao hawana uwezo wa kulipa Mawakili, tunawajengea uzalendo wa kusaidia Watanzania," alisema.

Njozi alisema katika kituo hicho wanatoa huduma za kisheria kwenye masuala ya mirathi, migogoro ya ndoa, ardhi na madai.

"Natoa wito kwa Watanzania wote waje kwenye maonesho haya ya wiki ya sheria lakini watembelee ofisi zetu zilizopo Dar es Salaam, tunatoa huduma za msaada wa kisheria bure kila siku ya Jumanne na Ijumaa," alisema.

# Ukosefu wa fedha wakwamisha ujenzi hospitali mkoa wa Mara

**Na Munir Shemweta,** MUSOMA

KUCHELEWA kupelekwa fedha katika mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mara, eneo la Kwangwa kumesababisha Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kutokamilisha mradi huo kwa wakati, imebainika.

Mradi wa ujenzi wa hospitali hiyo ulianza kujengwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) Septemba 15, 2019 na kutarajiwa kukamilika Agosti, mwaka jana.

Hata hivyo NHC ambayo ni mkandarasi, iliomba kuongezewa miezi sita kutokana na kazi zilizoongezeka nje ya mkataba pamoja na kuchelewa kupatikana makandarasi maalum wa mradi.

Akiwa katika ziara ya siku moja katika mkoa wa Mara juzi, kukagua utendaji wa sekta ya ardhi na kuhamasisha ukusanyaji kodi ya pango la ardhi, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alielezwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara, Catherine Mlapura, kuwa awali mradi huo ulikuwa ukiendelea vizuri, lakini kasi imepungua kutokana na NHC kutopatiwa fedha za kutekeleza mradi huo kwa wakati na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

"NHC imefanya kazi kubwa ikiwamo kutumia fedha za shirika kuharakisha ujenzi wa hospitali, lakini sasa tangu Bawa C (Wing C) kuanza kutoa huduma za mama na mtoto, kazi imesimama tangu Juni, 2020," alisema Katibu Tawala.

Mhandisi wa Mradi wa Ujenzi wa Hospitali hiyo, Renard Kazoba, alimweleza Naibu Waziri wakati akikagua mradi huo kwamba changamoto kubwa ya kutokamilika mradi huo kwa wakati ni kuchelewa kwa malipo.

Kazoba alisema pamoja na mkandarasi kuidhinishiwa malipo ya Sh. 3,591,565,635.35 ili kuharakisha utekelezaji mradi na kutakiwa kulipwa ndani ya siku 28 kwa mujibu wa mkataba, hadi sasa hakuna kiasi kilicholipwa.

Alibainisha kuwa katika kukabiliana na changamoto aliyoainisha, NHC imefanya vikao na wahusika wakuu wa mradi na kutolea mfano wa kikao kilichofanyika Novemba 6, mwaka jana, baina ya shirika na wahusika hao na kukubaliana mambo ambayo shirika linasubiri utekelezaji wake.

Aidha, Kazoba alisema NHC imenunua jenereta yenye uwezo wa 250 KVA pamoja na vifaa vya kuiwezesha kufanya kazi kwa kutumia fedha za ndani ili kufanikisha upatikanaji umeme wa uhakika katika jengo la Bawa C.

Dk. Mabula alisema ili NHC itekeleze majukumu yake ipasavyo, inahitaji kupata fedha kwa wakati kupitia miradi inayotekeleza hasa ikizingatiwa haipokei ruzuku kutoka serikalini. Alisisitiza kuwa isipowezeshwa itashindwa kutekeleza miradi yake.

Alisema katika utekelezaji mradi wa ujenzi wa hospitali hiyo, NHC inatakiwa kukamilisha kwa gharama ya Sh. 15,082,481,832.82 na hadi sasa imelipwa Sh. 8,469,851,800.34 na kiasi kilichobaki ni Sh. 6,612,630,032.48.

Pia alisema katika kutekeleza mradi huo, NHC imetumia fedha zake za ndani Sh. 3,591,565,635.35 na kusisitiza kiasi hicho kisipolipwa shirika litashindwa kufanya kazi.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa, Dk. Lazoro Mwikabe, alisema tangu hospitali hiyo kuanza kutoa huduma katika sehemu ya Bawa C, zaidi ya watoto 1,000 wamezaliwa na wananchi wa mkoa wa Mara wana imani kubwa na huduma za hospitali hiyo.

Aliongeza kuwa hospitali imejipanga na iko katika mazungumzo na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHF) ili kupatiwa mkopo wa kununua mashine ya CT Scan.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Butata, Musoma Vijijini mkoani Mara, wakipanga vitabu kwenye maktaba mpya ya shule hiyo, iliyojengwa na Shirika la Kimataifa linaloshughulikia lishe bora shuleni la Project Concern International (PCI Tanzania). . **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TBS yateketeza bidhaa za mil. 40/-

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limeteketeza bidhaa zenye thamani ya Sh. milioni 40 zisizokidhi ubora wa viwango.

Bidhaa hizo zimeondolewa sokoni na wakaguzi wa TBS Kanda ya Kati kuanzia Novemba, mwaka jana, hadi Januari 15, mwaka huu, katika mikoa ya Dodoma, Tabora na Singida.

Akizungumza baada ya uteketezaji wa bidhaa hizo katika dampo la Chidaya, Mkurugenzi wa Udhibiti wa Ubora wa TBS, Lazaro Msasalaga, alisema bidhaa zilizoharibiwa ni pamoja na vipodozi vyenye viambata vya sumu, vyakula na vinywaji ambavyo muda wake wa matumizi umepita, vilivyopatikana katika mikoa hiyo ya Kanda ya Kati.

"Katika kulinda afya za walaji, TBS tumekuwa tukifanya ukaguzi katika miji yote nchini kupitia kanda zatu sita na kila wiki tunafanya ukaguzi na kuteketeza kwani huu utaratibu ni endelevu. Ili wafanyabiashara wasipate hasara, ni vyema kuangalia kila wakati bidhaa zao na kuhakikisha wanaziuza kabla ya muda au kuwasiliana na TBS ili tuviteketeze bure.

"Ukiangalia asilimia kubwa ya bidhaa tulizoteketeza ni vyakuka vya watoto. Hii ina maana kwamba tusipokuwa makini tutatengezeza taifa la baadaye lenye matatizo ya kiafya. Hivyo jamii pia inatakiwa kushiriki katika vita hii kwa kukagua muda wa matumizi ya bidhaa wanazonunua," alisema.

Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009 pamoja ya Sheria ya Fedha Na. 8 ya mwaka 2019 mbali na majukumu mengine, zimeipa mamlaka TBS kuondoa bidhaa hafifu sokoni na kuziharibu au kuzirudisha zinakotoka pindi zinapobainika kuwa hazifai kwa matumizi ya binadamu.

Naye Mkuu wa Uhusiano wa TBS, Roida Andusamile, alisema wakaguzi wa TBS hufanya ukaguzi wa bidhaa viwandani na sokoni ili kujiridhisha na hali halisi ya soko na inapobainika uwepo wa bidhaa hafifu huondolewa sokoni na aliyekutwa na bidhaa hizo analipia gharama za uteketezaji.

Aidha, Andusamile alitoa rai kwa wafanyabiashara wote kuhakikisha kuwa wakati wote wanazingatia masuala ya ubora kwa kuuza bidhaa za vipodozi na vyakula vilivyosajiliwa pamoja na ukomo wa matumizi wa bidhaa hizo ili kulinda mlaji na kuepuka hasara.

"Pia wafanyabiashara wote wametakiwa kusajili bidhaa za vyakula, vipodozi, majengo ya kufanyia biashara na maghala ya kuhifadhia," alisema.

# Watakiwa kupeleka migogoro barazani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WATANZANIA wameshauriwa kulitumia Baraza la Ushindani (FCT), kuwasilisha migogoro yao ya kibiashara ambayo hawajaridhika na uamuzi uliofanywa na taasisi mbalimbali ili kupata haki.

Akizungumza jana kwenye maonyesho ya Wiki ya Sheria na Miaka 100 ya Mahakama yanayofanyika jijini hapa, Mwenyekiti wa Baraza hilo, Jaji Stephen Magoiga, alisema baraza hilo limekuwa likitoa uamuzi wa kesi mbalimbali na wananchi wanapata haki zao bila vikwazo.

"Baraza hili ni la muda mrefu na lina miaka mingi limeanzishwa tangu 2003, na migogoro inayokuja kwetu inakuwa kwenye hatua ya rufani maana vyombo vinavyopaswa kushughulikia ngazi ya chini huwa vimetoa uamuzi, hivyo mtu asiporidhika ndipo anakuja kwetu. Tunawakutanisha wote hadi aliyetoa uamuzi na baraza hutenda haki kwa kuzingatia sheria," alisema.

Alisema baraza hilo ni chombo muhimu kipindi hiki cha Tanzania ya viwanda ili kuondokana na tabia ya kiwanda kutoa bidhaa ya kiwanda kingine.

"Katika kusikiliza kesi hizi hakuna mlolongo ni hatua moja inaisha, tumefanya hivi ili kutoa uamuzi haraka watu waende kufanya biashara. Hiki ni chombo muhimu hasa wakati huu wa viwanda unaweza kutoa sabuni hii mtu mwingine akaja kukopi na kutoa kama ile ile," alisema.

Pia aliwasisitiza wafanyabiashara wanaotoka nje ya nchi kuzingatia sheria na masharti yaliyowekwa ili kusiwe na mgongano kwenye biashara.

Alisema wamekuwa wakipokea malalamiko kutoka mikoa mbalimbali nchini na lengo la baraza ni kuhakikisha watu wanafanya biashara bila kufanyiana roho mbaya.

"Kwa mfano TANESCO (Shirika la Umeme Tanzania) wanatupatia huduma ya umeme. Wamekupatia huduma ambayo haifai unalalamika, uamuzi utafanyika ambao huridhiki nao unakuja kwetu. Kuna mwingine amekuja kutoka Tanga anasema TANESCO hawajamwekea umeme wakati amekidhi vigezo. Tulitoa uamuzi na kuagiza TANESCO imwekee umeme," alisema.

# Idara afya Bahi mikononi mwa TAKUKURU

**Na Augusta Njoji,** BAHI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imeagizwa kuchunguza kwa miezi sita, Idara ya Afya ya Halmashauri ya Wilaya ya Bahi kutokana na kuwapo malalamiko kutoka kwa wananchi, ikiwamo wanafunzi kutozwa fedha kwa ajili ya kujaziwa ripoti ya afya.

Inadaiwa kuwa wanafunzi hao wanalipishwa kati ya Sh.5, 000 hadi 30,000 kwa ajili ya kujaziwa ripoti ya afya pindi wanapotaka kuripoti shuleni.

Malalamiko mengine ni ukosefu wa dawa, kutotumia mashine za kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato, wagonjwa kutozwa fedha kwa ajili ya gari la wagonjwa na baadhi ya wataalamu wa afya kuripoti kazini wakiwa wamelewa.

Agizo hilo lilitolewa na Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo katika kikao chake kilichofanyika juzi wilayani hapa.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Donald Mejitii, alisema idara hiyo imesababisha uwapo wa malalamiko mengi.

Alisema kila siku wanahamasisha wananchi kujiunga na mfuko wa afya ya jamii ulioboreshwa, lakini wakienda kwenye vituo vya afya wanaambiwa dawa hakuna.

"Rais Magufuli amejitahidi sana katika sekta ya afya, fedha za dawa zimeongezeka, lakini kiuhalisia baadhi ya watendaji huku chini wanamwangusha sana. Wanawatesa wananchi kwa kuwakosesha dawa ilhali tunawahamasisha wajiunge na CHF ili wapate huduma. Hapa utaona kabisa adui namba moja wa CHF ni wataalamu wetu," alisema.

"Kuna usemi kwamba 'The speed of the team is the speed of the leader'. Huu ndio ukweli, kama walio juu hawaendi na kasi walio chini yao hawawezi kuwapita. Haiingii akilini idara yenye malalamiko hivi lakini hata siku moja haijawahi hata kuleta onyo kwa watumishi au barua ya kuomba kuchukuliwa hatua ili baraza liidhinishe, haiwezekani," aliongeza.

Kwa upande wake, Mbunge wa Bahi, Kenneth Nollo, alisema kama baraza ni vyema wakaazimia kwa pamoja kuwa TAKUKURU wachunguze na watoe ushauri.

"Tuwaombe wenzetu TAKUKURU washauri kitaalamu wanaudhibiti vipi huo udokozi na mkuu wa utawala asaidie kurekebisha hii idara," alisema.

Awali, Diwani wa Ibugule, Blandina Magawa, alishauri idara hiyo kuangaliwa vizuri kwa kuwa inaonekana watumishi wanaonekana kuna mahali wanajivunia.

Naye Diwani wa Bahi, Augustino Ndonuu, alisema kuna ukosefu wa mashine za kielektroniki (POS) kwenye vituo vya afya, hivyo kusababisha halmashauri kukosa mapato yake.

"Ukienda kwenye vituo hakuna hizo mashine, baadhi ya watumishi wanapata mwanya wa kufanya wizi. Mgonjwa anaenda na pesa taslimu ya matibabu, lakini ukichunguza utakuta amewekwa upande wa wagonjwa wanaotibiwa kwa CHF. Hapa ujue tayari wizi umefanyika," alisema.

Akijibu malalamiko hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Dk. Fatma Mganga, alisema kwa mujibu wa sera ya afya mgonjwa hapaswi kutozwa fedha kwa ajili ya gari la wagonjwa.

"Katika dawa tukihamasisha pia wananchi wengi wajiunge na CHF itasaidia sana katika upatikanaji wa dawa maana fedha itakuwapo, lakini katika suala la watumishi sio la DED peke yake kuwaadabisha bali pale unapoona lete taarifa ili nijue na kuchukua hatua," alisema.



Diwani wa Kata ya Haneti Halmashauri ya Chamwino, Abdi Kagame, akizungumza wakati alipokuwa kwenye kujadili hoja mbalimbali za maendeleo kwa ajili ya wananchi katika kikao cha Baraza la Madiwani cha robo ya pili kwa mwaka 2021 kilichofanyika Chamwino jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**.

# TARI yawataka wakulima kuzingatia ushauri

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Hombolo, kimewataka wakulima wa zabibu kuzingatia ushauri wa wataalamu, ili kuepuka kupoteza mazao mengi shambani msimu wa mavuno.

Mtafiti wa TARI, Andekelile Mwamahonje, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari juu ya umuhimu wa wakulima wa zao hilo kuzingatia elimu ya uandaaji shamba, kupanda hadi kuvuna wanayopewa na wataalamu.

Mwamahonje alisema baadhi ya wakulima hawajui matumizi ya mbegu bora.

"Kuna baadhi ya hatua wakulima hawazijui ndiyo maana huwa tunaenda kutoa elimu kwa wakulima katika baadhi ya maeneo, ili kuwasaidia wasipoteze zabibu nyingi shambani kipindi cha mavuno," alisema Mwamahonje.

Alisema tayari walishatembelea wakulima wa wilaya mbalimbali zikiwamo Chamwino na Bahi kwa ajili ya kutoa elimu kwa wakulima wa zao hilo, ili kuhakikisha wanafanya vizuri ifikapo msimu wa kilimo.

Hata hivyo, alisema moja ya mikakati ya kituo hicho ni kuhakikisha wanatoa elimu kwa wakulima hao kwa kuwa ni zao la kibiashara ili kuwa na kilimo chenye tija.

"Tunaomba wakulima wazingatie elimu inayotolewa na kituo cha utafiti wa kilimo, tunahitaji kuona wakulima wa zao hilo mkoani hapa wanapiga hatua katika kilimo hicho," alisema Mwamahonje.

Alisema zabibu haifanani na mazao mengine na inachukua muda mrefu, hivyo mkulima anapaswa kufuata taratibu ambazo watafiti wameelekeza ambazo zitawapa manufaa makubwa katika kilimo.

Naye Mary Stephene, kutoka Idara ya Mbegu kituo hicho, alisema wamekuwa wakifanya jitihada za kuhakikisha wakulima wa zabibu mkoani hapa wanakuwa mfano wa kuigwa na wakulima wengine.

Alisema Dodoma ni mkoa pekee ambao zao hilo linalimwa misimu miwili, hivyo wakulima wanatakiwa kupata elimu mara kwa mara ya uandaaji mpaka uvunaji wa zao hilo.



HABARI ZANZIBAR

# ACT yapongeza mkataba Oman

**Na Hawa Abdallah,**

ZANZIBAR

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimepongeza hatua ya utiaji saini mkataba wa makubaliano baina ya Oman na Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) juu ya ujenzi wa bandari jumuishi huko Mangapwani, Kaskazini mwa Zanzibar.

Katibu wa Idara ya Habari, Uenezi na Uhusiano Kwa Umma wa ACT-Wazalendo, Salim Bimani alisema jana kuwa hiyo ni hatua kubwa na muhimu kwa ajili ya uchumi na ukuaji wa Zanzibar.

Utiaji saini wa makubaliano hayo uliyofanywa na Katibu Mkuu wa Wizara Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Amour Hamil Bakari, na kwa upande wa Oman alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji cha Oman, Sheikh Mohammed Al-Tooqi, ambaye aliongoza ujumbe kutoka mamlaka hiyo.

Chini ya makubaliano hayo, Oman imeweka nia kujenga bandari kadhaa kama vile ya mizigo na makontena, petroli na gesi, uvuvi na kuwapo chelezo kwa ajili ya matengenezo ya meli za ndani na nje katika ukanda huo.

Pia katika bandari hiyo kutakuwa na eneo la viwanda, eneo la biashara na makazi ya kisasa na Rais Dk. Hussein Mwinyi amesema huu ni mwanzo mzuri kwa Zanzibar.

"Lengo letu ni kuleta mabadiliko makubwa kwa maslahi mapana ya nchi yetu na fursa na faida kwa watu wote," alisema Bimani.

ACT-Wazalendo imewataka wananchi wote wasimame na SUK kwa umoja wao ili kuitia hima katika kuijenga Zanzibar.

"Kila tukishikamana ndiyo tutaipa nguvu SUK kufanya kazi na nchi mbalimbali na kampuni mbalimbali. Tunaamini mazingira mazuri zaidi yataandaliwa kushawishi wawekezaji zaidi," alisema Bimani.

# Waziri ataka vyanzo mbadala mapato

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Jamal Kassim Ali, amesema iko haja ya kutafuta njia mbadala ya kutafuta vyanzo vingine vya mapato katika serikali badala ya kutegemea utalii pekee.

Jamal aliyasema hayo jana katika ukumbi wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Vuga, alipokuwa akizungumza na Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi, iliyotaka kujua utendaji wa wizara hiyo.

Sekta ya utalii, alisema ndiyo tegemeo kubwa katika kuingiza pato la serikali, lakini inapotokea changamoto ndani ya nchi na watalii kuwa hawaji kama vile kipindi cha corona, uchumi kwa asilimia kubwa unakuwa chini.

Alisema serikali ya awamu ya nane chini ya Rais Hussein Mwinyi, imedhamiria kufanya mabadiliko makubwa kwa wafanyabiashara ili kulipa kodi kwa mtindo wa kielektroniki kwa lengo la kuongeza mapato ya serikali.

"Lazima wananchi wapatiwe elimu ya kuwekeza katika vyanzo vingine kama uchumi wa buluu. Wafanyabiashara walipe kodi kama inavyotakiwa, hivyo itawezesha kuongezeka uchumi wa taifa na kupatikana maendeleo zaidi," alisema.

Pia alisema nchi yoyote ili iwe na maendeleo ni lazima ikusanye kodi kwa kuwa bila kulipa kodi haiwezi kupata maendeleo ambayo ndiyo dhamira ya serikali katika kukuza uchumi na kuwapatia huduma wananchi wake kama vile kulipa mishahara kwa wakati na mambo mengineyo.

Nao wajumbe wa Kamati ya Bajeti, wakitoa michango yao ya taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya serikali kwa kipindi cha miezi sita Julai hadi Desemba, 2020, waliishauri serikali kuwataka makandarasi wanaochukua dhamana ya kusimamia miradi ya maendeleo iende kwa wakati.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Saada Mkuya Salum, alisema changamoto kubwa iko katika ukusanyaji wa mapato kutokana na wafanyabiashara wengi kulalamikia wingi wa kodi, hivyo kuna haja ya kurahisisha mfumo wa elektroniki ili kudhibiti mapato kuingia kunakostahiki.



Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Prof. Shadrack Mwakalila, akielezea azma ya uongozi wa chuo hicho, kampasi ya Karume utaratibu wa kuanza ujenzi wa majengo ili kuwaondolea usumbufu wanafunzi wake. **PICHA: OMPR.**

# Hemed aipa tano Mwalimu Nyerere

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema serikali inathamini mchango wa vyuo vinavyotoa elimu nchini akitolea mfano wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, kinachoendelea kutoa wataalamu wa kadi tofauti.

Hemed aliyasema hayo jana alipofanya mazungumzo na uongozi wa chuo hicho, alipokutana nao ofisini kwake, Vuga jijini Zanzibar na kuupongeza kwa maono yao ya kuanzisha kampasi Kisiwani Pemba.

Alisema hatua hiyo muhimu itasaidia zaidi wananchi hasa vijana wa Zanzibar kuendelea kupata taaluma kwa urahisi zaidi.

Mafanikio yaliyopatikana ndani ya chuo hicho, alisema yanatokana na ushirikiano wa kina na kuuhakikishia uongozi wa chuo kwamba serikali itaendelea kuwaunga mkono, huku ikitaka nguvu za ziada katika kukikuza chuo ili kizidi kukuza taaluma.

Alibainisha kwamba Watanzania wanaendelea kufaidi matunda ya chuo hicho, hivyo iko haja ya kutanua wigo wa elimu kwa vile wahitimu wa taasisi hiyo tayari wanatumika katika sekta mbalimbali za serikali na hata zile binafsi.

Hemed ameelezea faraja yake kutokana na kasi ya taasisi hiyo ya elimu inayokwenda sambamba na utayari wa awamu ya nane wa kuleta maendeleo kwa wananchi, ikiwategemea zaidi wasomi hao.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Shadrack Mwakalila, alisema wanafunzi na hata wakufunzi wa chuo wamekuwa wakikabiliwa na changamoto ya ukosefu wa dakhalia.

Katika kukabiliana na tatizo hilo linalochangia kupunguza muda wa masomo, Prof. Mwakalila alisema uongozi umeshaandaa utaratibu wa kuanza ujenzi wa majengo ya dakhalia yatakayotoa huduma kwa wanafunzi 1,960.

Aidha, Prof. Mwakalila alisema licha ya kuwapa elimu wanafunzi chuoni hapo, pia wanawajenga kuwa na uelewa wa uongozi na maadili pamoja na mbinu za kujua namna bora ya kujiajiri ili kuondokana na dhana ya kusubiri ajira serikalini.

Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Kampasi ya Karume, Zanzibar, kilianza na wanafunzi 22 mwaka 2013 na hadi mwaka jana kilikuwa na wanafunzi 1,920.








SUKARI TUPU

# Utadambua wee... Zuchu hatari

MWANAMUZIKI anayefanya maajabu katika muziki wa Bongo Fleva, Zuchu, yupo mbioni kuvunja rekodi nyingine baada ya wimbo wake 'Sukari' kuwa maarufu kati ya nyimbo zote zilizotambulishwa mwezi Januari.

Wimbo huo ambao mpaka juzi umetazamwa zaidi ya mara milioni 2.2 katika mtandao wa You Tube, umezidisha joto kwa mashabiki wa muziki kutokana na mtindo wa uchezaji wake.

Watu wameonekana kupagawa na aina ya uchezaji wake ambao kuna sehemu unamfanya mtu kuganda kama roboti pamoja na lugha iliyotumika kuwa ya kitaalamu zaidi.

Aidha, baadhi wa wataalamu wa Kiswahili, wanasema msanii huyo ametumia maneno ya ndani ambayo yalikuwa yanatumiwa na wasanii wa Taarab na washairi wa kale.

"Wimbo wa 'Sukari' Kiswahili chake kimetumika cha ndani na si rahisi mtu kufahamu ana maana gani, ufundi huu ulikuwa ukitumiwa na waimbaji wa taarabu na washairi wa zamani, amesema Aisha Jumbe.

Amesema ladha ya wimbo wa Kiswahili lazima uwe na maneno ya kificho, na ndivyo Zuchu alivyofanya na kusababisha kila mtu kutoa maana yake anayojua.

"Maneno kama 'ladha yake msala, shira ya Kizanzibari' hapa unatakiwa kutafakari kujua maana halisi," ameongeza kusema.

BASI SAWA

## Jux kaanza mwaka vizuri

MWAKA 2021 umekuwa mzuri kwa mwanamuziki wa miondoko ya R&B nchini, Juma Jux, maarufu kama Jux baada ya kutambulisha mjengo wake mpya.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Jux aliweka video fupi ikionyesha mandhari ya jumba hilo la kifahari huku akiandika maneno 'Mwaka Mpya, Nyumba mpya".

Jumba hilo la kifahari limeanza kuwa gumzo huku mashabiki wake wakimpongeza kwa kupiga hatua kubwa na hatimaye kumiliki makazi ya gharama.



## Mbosso amshukuru Rich Mavoko

MWANAMUZIKI kutoka lebo ya WCB, Mbwana Kilungi, maarufu kama Mbosso, amesema kama sio Rich Mavoko, maisha yangu yangebaki kuwa ya kuganga njaa kila siku.

Amesema baada ya kundi la Ya Moto Band kuvunjika, alirudi kijijini kwake Kibiti, huko alijiingiza katika uchezaji wa soka kama njia ya kusaka maisha mapya.

Alisema siku moja alikwenda Rich Mavoko na kufanya mazungumzo, na hapo ndio ilikuwa safari yake ya kusaini WASAFI.





## Lady Jaydee kumbe umewashtukia

MSANII mkongwe wa Bongo Fleva, Lady Jaydee, amesema watu wamegeuza kauli yake ili kumtia ubaya kwa mwanamuziki mwenzake Ali Kiba.

Kauli hiyo inatokana na ile ambayo alimjibu shabiki wa Twitter, aliyemuuliza kama anatamani kufanya kazi tena na Alikiba? Katika jibu lake Lady JayDee alisema hataki na haitatokea kufanya kazi na msanii huyo.

"Naona kama kuna ubaya umetengenezwa na watu ili nionekane nimekataa kufanya kazi na Ali Kiba, lakini jibu langu nilimaanisha siwezi kwa sababu sijazungumza naye kwa karibu miaka minne sasa," amesema Lady Jaydee.

## Shemeji; ukimgeuza geuza nyoka utaona miguu yake

**Na Adam Fungamwango**

WAPARE wana msemo mmoja maarufu 'ukimgeuza geuza nyoka utaona miguu yake.'

Maana na msemo huu ni kwamba ukimchokoza sana mtu mpole kwa kutegemea kuwa hatokufanya kitu, ipo siku isiyo na jina atakubadilikia na utashangaa kama ni yeye au mwingine.

Maana nyingi ni kwamba ukilitafuta sana kosa, basi utalipata tu. Mfano wale wanaume na wanawake wanaopenda sana kukagua simu za wake au waume zao. Ipo siku watakutana na wanachokitafuta.

Leo tunaiangalia filamu ya 'Shemeji'. Filamu hii inamhusu kilana Adam ambaye aliamua kumpeleleza mkewe ajue kweli anampenda au la.

Kutokana na hilo, akapanga dili na rafiki yake Hans kuwa amtongoze mkewe Sonia, lakini awe anampelekea mrejesho.

Na kweli, Hans akamtongoza mke wa rafiki yake Adam kama alivyoambiwa. Kwanza alikataliwa.

Baadaye akaambia ngoja akafikiri. Baadaye akakubaliwa. Na mara zote hizo, Hans alikuwa akipeleka mrejesho kwa rafiki yake.

Adam alishangaa sana kuona mkewe anaonekana kukubali, wakati nyumbani anaonekana anampenda sana na hana mwanaume yeyote yule.

Kila siku zinavyozidi kusonga mbele, ndipo Adam anapopata habari mbaya kutoka kwa mkewe kutoka kwa rafiki yake Hans.

Mpaka siku ikafikia kuwa wamekubaliana wakamalize mchezo nyumbani kwake.

Alichokitaka sasa amekipata. Lakini akamsihi rafiki yake asifanye kweli, amdanganye tu.

Kilichofanyika ni kwamba mke anamdanganya mume kuwa anakwenda kwa shoga yake, kumbe anaenda kwa mwanaume. Mwanaume mwenyewe ni yule rafiki yake. Adam akakubali.

Mke akaenda hadi huko. Hans alimpigia simu rafiki yake bila mwanamke kujua na simu akaiacha wazi ili awe anasikiliza kila kitu. Hans akamuuliza kwa nini ameamua kumsajili mumewe. Mke akasema wazi ni kwa sababu ana upungufu wa nguvu za kiume.

Hans alidanganya kuwa amepigiwa simu na asingeweza kufanya lolote, hivyo Sonia akarejea nyumbani.

Ukazuka ugomvi mkubwa na mkewe, lakini ni ukweli kuwa Adam alikuwa na tatizo hilo, hivyo akaamua kulitibu. Alipopona ndoa ikarejea kama kawaida, ikawa ya amani na utulivu.





## Irene aapa 'Sitalia' tena


MWIMBAJI wa nyimbo za injili nchini, Irene Robert ametambulisha video ya wimbo wake mpya inayojulikana 'Sitalia' akimshirikisha Christina Shusho.

Akizungumza na BT, Irene amesema wimbo huo una maudhui mazuri yatakayotoa nguvu na ushindani kwa watu.

"Wimbo huo uko tayari katika mfumo wa audio na video, Mungu ameahidi kutulinda, kutufuta machozi na kutupigania dhidi ya maadui zetu, hivyo hatuna sababu ya kulia," amesema Irene.

Amesema baada ya kutambulisha wimbo huo, amejipanga mwaka huu kuachia nyimbo nyingine kwa kufanya kolabo na wasanii tofauti.





## Mwaka mpya sukari? Bado Sana

**Na Adam Fungamwango**

HUU sasa ni mwaka 2021 ambao umeingia huku baadhi ya wasanii nao wakiukaribisha kwa mbwembwe, wakitoa ngoma mbalimbali.

Kila msanii angependa mwaka mpya atoe ngoma ambayo ingeanza kuwa gumzo na kujikusanyia mashabiki ambao wangeendelea kumpa sapoti kwa mwaka mzima.

Leo tunaziangalia ngoma ambazo zimetolewa mwaka huu na zimeanza kuwa gumzo kwa mashabiki ambapo mbali na kuangaliwa na watu wengi kwenye mitandao ya kijamii, lakini imekuwa ikiombwa na kupigwa sana kwenye vituo vya televisheni na redio.

**Bado Sana - Lavalava ft Diamond**

Ilikuwa ni sikukuu ya mwaka mpya, yaani tarehe moja Januari 2021 wakati msanii Lavalava alipochomoa ngoma yake moja kati akimshirikisha mkali Diamond Platinumz aliyoiita "Bado Sana."

Ni ngoma ambayo kwa sasa 'imetrendi' sana kila unapopita. Hata video ya ngoma hiyo imeonekana kupendwa mno kutokana na kuchukuliwa kwenye mazingira halisi ya Kiswahili.

Moja kati ya maneno yanayopendwa sana na mashabiki wenye ngoma hiyo ni yale yanayoimbwa na Simba mwenyewe.

"Kuimba wataimba, lakini kumfikia, bado sana." "Niache kula bata eti Simba uoe, bado sana."

**Baba - Stamina ft Profesa Jay**

Kukaja na mapinduzi mapya ya muziki wa kizazi kipya, kuirudisha kule mwanzo kwenye kuimba ngoma za mafunzo kwenye jamii, badala ya ngoma za mapenzi ya chumbani.

Stamina akimshirikisha mkongwe, Profesa Jay, Januari 13, wakaibuka na ngoma moja iiitwayo 'Baba'. Ni ngoma inayoonyesha kuna mgogoro kwenye familia fulani hivi, baba na kijana wake wakitofautiana kauli.

"Ungemrubuni mama angeolewa na mwanaume mwenye pesa. Mzee Mushi, Mwakalinga, Rukashobya wote wana pesa, wewe ulikuwa wapi hadi unakuwa maskini?" Ni kijana anamzodoa baba yake ambaye naye akajibu

"Kwanza haikuwa damu yangu, hivyo nilikulea na sikutaka isimuliwe na wewe usijue, lakini watoto wenzako wote wamesoma, wewe umekataa shule. Aliyekwambia usisome nani?"

**Infidele - Ali Kiba**

Msanii maarufu nchini, Ali Kiba naye hakuwa nyuma kuukaribisha mwaka mpya na ngoma mpya. Yeye akaja na ngoma moja ya mapenzi Januari 18 aliyoiita 'Infidele.'

**Anajikosha - Harmonize**

Harmonize naye hakuwa nyuma. Januari 20 na yeye akafyatua ngoma yake mpya aliyoiitwa 'Anajikosha'. Sijajua kama ni dongo au ni nini.

Lakini moja kati ya mashairi yake ni pale anaposema 'Jumamosi analewa, halafu Jumapili anakwenda kanisani, huyo anajikosha."

**Sukari - Zuchu**

Zuchu ameingia kwenye rekodi ya kuwa msanii wa kwanza wa kike aliyetoa ngoma kwa mwaka huu mpya, ikahiti.


'Sukari' ndiyo kwa sasa habari ya mjini.

"Eti nimemlambisha, ananiambia chombeza.

"Tena niliizidisha, ananiambia koleza. Nikitaka kusitisha, ananambia ongeza.

Japo imethibitishwa, ila itampoteza.

Ikipanda ni balaa, ikishuka ina madhara."



# Wasanii Afrika wamlilia Larry King

WASANII maarufu barani Afrika wamejitokeza kuonyesha simanzi zao kutokana na kifo cha mwanahabari anayeheshimika duniani, Laryy King.

Mwigizaji mkongwe wa Nigeria, Joke Silver, ameandika kupitia ukurasa wake wa Instagram kwamba "Pumzika kwa amani Larry King. Wewe ni mfalme wa mahojiano, kila siku nakuheshimu na siku zote nakusikiliza."

Mchekeshaji maarufu Gbenga Adeyinka, amesema "mkongwe hujafariki, unapitia kwenda mbinguni, pumzika kwa amani Larry King". Ameandika.



## Halsey kajazwa ujauzito

MSANII na mwandishi wa nyimbo kutoka Marekani, Halsey, ametoa taarifa nzuri kwa mashabiki wake kuwa yeye ni mjamzito.

Halsey (26) kupitia ukurasa wake wa Istagram, ameposti picha ikimwonyesha tumbo lake na kusababisha mashabiki wake kumpongeza.

Bado haijajulikana nani baba wa mtoto huyo, lakini inahisiwa yawezekana mimba hiyo ni ya Alev Aydin.

## Giza latanda tena Nollywood

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Ernest Asuzu, amefariki dunia baada ya kupatwa na shinikizo la moyo.

Asuzu ambaye anajulikana kama 'Bad Boy. Alifariki Jumanne akiwa usingizini.

Mke wa mwigizaji huyo, Jennifer, alithibitisha kifo hicho na kueleza kuwa siku chache kabla ya kufariki, alikabiliwa na tatizo la shinikizo la moyo.





## Master KG hataki pesa Jerusalema

MTAYARISHAJI na mwanamuziki maarufu wa Afrika Kusini, Master KG, amesema kamwe hajapewa pesa na msanii Burna Boy, ili kuurudia kibao cha Jerusalema ambacho kimepata umaarufu duniani.

Master KG, ameliambia gazeti moja la Nigeria, kwamba katika mjadala wao wa kurudia wimbo huo hawakuzungumzia siala la malipo.


Amesema Burna Boy, alimwambia jinsi alivyovutiwa na wimbo huo na kuwa mmoja wa wafuasi sugu wa Jerusalema kutoka ndani ya moyo wake.

## Trey Songz matatani

MWANAMUZIKI wa Marekani, Trey Songz, amekamatwa baada ya kutuhumiwa kumshambulia ofisa wa polisi.

Tukio hilo limedaiwa kutoke Januari 24, katika uwanja wa Arrowhead Stadium, kabla ya kuanza mechi ya ligi ya mpira wa Kimarekani (NFL).

Kulingana na mashuhuda wanasema polisi ndiye aliyefanya makosa kwa kumvamia Trey, ndipo palitokea mabishano makali na kusababisha msanii huyo kumshambulia polisi.



# EWURA yaja na mwarobaini malalamiko ya ankra za maji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAJI ni uhai. Usemi huu huonyesha namna maji yalivyo muhimu kwa kiumbe hai chochote duniani.

Kutokana na umuhimu huo, serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kusogeza huduma ya maji kwa wananchi.

Hata hivyo, katika utoaji wa huduma hiyo, kero kubwa inayowakabili watumiaji kwa sasa ni kupatiwa ankra zikiwa na gharama kubwa ikilinganishwa na huduma waliyotumia. Ankra hizo hutolewa na mamlaka za maji za mikoa, wilaya, mji midogo na miradi mikubwa ya kitaifa.

Kutokana na kukithiri kwa malalamiko hayo, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imeamua kuja na mbinu nyingine mpya ya kielektroniki itakayokuwa mwarobaini wa kuondokana na tatizo la wateja kubambikiziwa ankra za maji.



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje (katikati), akizungumza wakati wa kutangaza kufuta bili mpya za maji hivi karibuni. Kushoto ni Mkurugenzi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa mamlaka hiyo, Mhandisi Exaud Maro, na Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA, Titus Kaguo. **PICHA: EWURA**

### MKURUGENZI EWURA

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje, alisema hivi karibuni kumeibuka wimbi la malalamiko hayo makubwa na kati ya malalamiko yote yanayopokewa na EWURA katika sekta za umeme, mafuta, gesi asilia, asilimia 60 ni ya maji.

"Kilio kikubwa kutoka kwa wateja wa huduma za maji kipo kwenye ankara za maji. Asilimia 75 ya malalamiko yote ni kutokubaliana na ankra zinazotolewa na mamlaka mbalimbali nchini," alisema.

Alisema malalamiko mengine ambayo ni makubwa na migogoro ya uunganishaji huduma za maji ambayo ni asilimia 13.

Hata hivyo, alisema licha ya EWURA kuchukua hatua ya kufuta bei za maji zilizopaswa kutozwa kuanzia Januari, mwaka huu, ili kufanya uchunguzi wa kina kutokana na kukithiri malalamiko ya kubambikiziwa ankra wateja, mamlaka hiyo inakuja na mfumo wa kielektroniki utakaoondoa malalamiko hayo.

Kwa mujibu wa Chibulunje, mamlaka hiyo inaendelea kutekeleza agizo la Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, la kutaka wananchi washirikishwe katika kusoma ankra za maji, ambapo wanatarajia kuja na mfumo huo wa kielektroniki ambao utashirikisha wasomaji wa ankra za maji na wateja.

"Kama mwananchi hatendewi haki lazima ifanyike kazi ya ziada na uchunguzi utafanyika na tutatoa taarifa baada ya kujiridhisha," alisema na kubainisha kuwa mfumo huo uko mbioni kukamilika na utaondoa malalamiko hayo kwa wananchi.

Kuhusu kufuta ankra za maji, Mhandisi Chibulunje alisema bei hizo zilizofutwa ni zile ambazo zilikuwa zimeidhinishwa na mamlaka hiyo kwa mwaka 2020/21 na kwa sasa zitaendelea kutozwa zilizokuwapo za mwaka 2018/19.

"EWURA huidhinisha bei kwa mamlaka za maji kwa miaka mitatu, ambapo bei hizo ziliidhinishwa kwa mwaka 2018/19, 2019/20 na 2020/21 na kwa utaratibu wetu kuanzia Januari 2021 mamlaka nyingi zilikuwa zinatarajia kuanza kutumia bei za mwaka 2020/21," alisema.

Hata hivyo, alisema kutokana na malalamiko hayo EWURA imefuta bei zote ambazo zilitakiwa kuanza kutumika mwezi huu na kuelekeza zitumike bei za mwaka 2018/19.

"Hatua hii inachukuliwa ili kuipa uwezo EWURA kufanya uchunguzi wa kina juu ya malalamiko haya ya maji, ili kubaini ukweli wa malalamiko hayo ambapo baada ya kumaliza shughuli ya uchunguzi wa kiufundi, EWURA itatoa maelekezo mengine ya matumizi ya bei ambazo zilitakiwa kuanza Januari, mwaka huu," alisema.

Awali, akifafanua mchakato wa uidhinishaji ankra hizo, Mhandisi Chibulunje alisema EWURA ina jukumu la kupitia gharama kama zina uhalali kwa kulinganisha na gharama za kipindi cha nyuma za mamlaka husika pamoja na hesabu za fedha zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

"Tunazingatia kulinda maslahi ya wateja, huduma kwa wasio na uwezo pamoja na uendelevu wa huduma husika, na pia tathmini ya mapendekezo ya bei huzingatia mlingano wa gharama za uendeshaji za mamlaka zingine za maji nchini," alisema.

Mkurugenzi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa EWURA, Mhandisi Exaud Maro, alisema bei za maji zinatofautiana kwa mamlaka za maji, huku akisema inatokana na gharama za usafirishaji wa maji kutoka kwenye vyanzo vya maji hadi kuwafikia wateja.

Alisema usafirishaji wa maji pekee unachukua asilimia 45 hadi 50 ya gharama za uendeshaji za mamlaka husika.

### KAULI ZA WANANCHI

Akizungumza na Nipashe kuhusu kero ya ankra za maji, Mkazi wa Dodoma, Anna Gelle, alisema kuna tatizo la kutozwa ankra tofauti na kilichotumika hali inayowakwaza wananchi na kushauri kufungwa kwa mita za malipo ya kabla ili kuondokana na kero hiyo.

Alisema wasomaji wa mita wamekuwa wakiingiza takwimu za uongo za mtumiaji bila kufika nyumbani na kusoma kiwango cha maji alichotumia.

"Maoni yangu ni kwamba wawe makini kwenye usomaji wa mita na uingizaji takwimu kwenye mifumo kwani mfumo hufuata 'command' ya mtu na sio upo automatic, mi naona tupatiwe tu mita za prepaid ili kuepusha haya malalamiko ya ankara za maji kukosewa au kutosomwa kwa usahihi," alisema.

Alisema licha ya kutumia maji yanayotoka mara mbili kwa wiki, ankra aliyoletewa inaonyesha matumizi makubwa ya maji ikilinganishwa na uhalisia wa namba zinazosomeka kwenye mita yake.

"Inashangaza mimi nimeletewa ankra ambayo inaonyesha usomaji uliopita ilikuwa 1808 na ilisomwa Januari 13, mwaka huu, inaonesha 1808 ambao cha kushangaza ankra imekuja inaonesha nimetumia uniti 18 natakiwa kulipa zaidi ya Sh.22,000 wakati kwa hesabu za kawaida hapo ni ziro, lakini leo nimeangalia mita yangu inasomeka 1817 sasa hizo takwimu wanatoa wapi?" Alihoji.

Naye Maria John alisema ankra zinatozwa bila wasoma mita kupita kwenye maeneo husika hilo ndilo linasababisha wateja walalamike kubambikiziwa ankra.

"Mimi kwangu tangu nimehamia sijamwona msoma mita. Sasa nashindwa kujua hizo ankra wanazotutoza wanasoma wapi. Kadi yangu haijajazwa kitu, tunataka wakija kusoma watushirikishe na kujaza ili tujue pia na kiwango cha maji tunachotumia," alisema.

### KAULI YA WAZIRI

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema kuna tabia ya watendaji wa mamlaka za maji kubambikiza ankra za maji wateja na kuagiza wasomaji wa mita washirikishe wananchi.

"Mwananchi analipia ankra ya maji anayotumia lakini hizi ankra zisiwe bambikizi lazima EWURA isimamie hili kuna bei za maji za mifukoni," alisema. "Pia kuna baadhi ya mamlaka ambazo zimekuwa zikitoa bei ya maji bila kuidhinishwa na EWURA. Naagiza EWURA kuhakikisha mnawajengea uwezo wakurugenzi na kutoa elimu ya wananchi ili kujua wapi kwa kwenda wanapokuwa na malalamiko yao ikiwamo kutokubaliana na ankra zinazotolewa," aliongeza.

Hata hivyo, anasema amezuia utekelezaji wa upandishaji ankara za maji hadi atakapoelekeza.

"Nazuia kwa muda utaratibu huu hadi hapo timu ya wataalamu wa wizara atakapoona kama kuna haja ya kupandisha bei ya maji, kazi ya EWURA si kupitisha ankr za maji bali ni kudhibiti na kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji kwa bei mwafaka na bila kubambikiziwa ankra," alisema.

# UMMA ULIVYOIPOKEA CORONA KWA NIDHAMU YA MWITIKIO, KUJIFUNZA

**Na Frank Monyo**

KULIPUKA na kusambaa kwa virusi vya corona mwanzoni mwa mwaka jana, kumesababisha watu duniani kubadili mfumo wa maisha.

Kulipotangazwa maradhi hayo nchini, wataalamu wa afya walitoa miongozo ya kuidhibiti isisambae. Ghafla mwitikio uliibua utamaduni mpya wa kunawa mikono, kutumia kitakasa mikono (sanitizer), barakoa, kujifukiza, mlo na uhifadhi wa chakula.

Pia hayo yalijitokeza katika masomo, ufanyaji kazi, biashara na mtandao wa mawasiliano, huku serikali kupitia wizara inayohusika na afya, ilichukua hatua kuelimisha afya kwa jamii.

Ni kinyume na zamani kuliposhuhudiwa kasi ndogo ya jamii kuelewa na kufuata maelekezo kulipotokea magonjwa makubwa ya mlipuko na mengineyo yenye athari kama vile ukimwi, kipindupindu, malaria na kifua kikuu.

Kwa tukio corona kumeshuhudiwa mwitikio na nidhamu ya kipekee kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya na serikali, hata kuipunguzia serikali jukumu.

KITAKASA MIKONO

Kutangazwa rasmi corona nchini, mgonjwa wa kwanza mkoani Arusha, Machi mwaka, iliendana na umma kufahamishwa sifa ya ugonjwa huo na unavyokabiliwa.

Darasa kutoka wizara inayohusika na afya, ilieleza mbinu mojawapo ni kutakasa mikono kwa maji tiririka. Watu walitii 'bila shuruti' mara moja, wakadumisha hata baada ya kutangazwa imetoweka.

Utakasaji mikono ukachukua nafasi kila nyumba, uswahilini kwa uzunguni, palipo na wapangaji hali kadhalika penye familia; ndoo na 'sanitizer' zikipatikana.

Kuna watu kabla kutangazwa hawakuyajua hayo na kama walijua hawakutumia. Kimsingi, inaua wadudu, jambo ambalo ni muhimu hata katika vita kama vya kipindupindu.

Nyenzo 'sanitizer'na kunawa mikono vimekuwa kwenye maeneo ya umma kama vituo vikuu vya daladala, hospitali, sokoni, ofisni, shule na majumbani.

**MAISHA YA BARAKOA**

Ni nani leo asiyeijua, mkubwa kwa watoto? Je, hivi sasa unaweza kutembea umbali mkubwa pasipo kuona mvaaji barakoa?

Imekuwa nyenzo ya afya inayosaidia kupunguza uwezekano mtu kuambukizwa au kuambukiza magonjwa yanayosamba kwa njia ya hewa, mathalani virusi kupitia mate na majimaji kupitia maongezi, kukohoa na kupiga chafya.

Barakoa imeshakuwa vazi la kawaida, ingawa haina maana ni mpya sana. Imetumika ama kuzuia au kupunguza athari na hatari za vumbi, gesi, hewa chafu au viini vya ugonjwa.

Tafsiri yake ya asili, ni mbadala wa kanuni ya afya mtu ya kuziba mdomo kwa kutumia kiwiko cha mkono, kitambaa au viganja na tangu corona, matumizi ya yake yameongezeka sana nchini na duniani.

## ●Kila agizo 'ndiyo'; weledi, wabunifu



Wanafunzi waliovaa barakoa, wakinawa kwa maji tiririka na vitakasa mikono ikiwa ni namna ya kujihami dhidi ya virusi vya corona. **PICHA MTANDAO.**

Ni funzo lililopo siku nyingi, mashahidi mojawapo ni wanaougua maradhi ya kifua kikuu, kuwalinda majirani na maambukizi, pia sehemu ya ustaarabu wa jamii walio karibu kujaliana kifya.

**KUJIFUKIZA**

Mapema mwaka jana, Rais Dk. John Magufuli alisema mwanawe alipatwa na virusi vya corona na akapona kwa kujitenga, kunywa malimao na kujifukiza.

"Alijifungia kwenye chumba huko akaanza kujifukiza, akanywa malimao na tangawizi, amepona yuko mzima...," alitamka kutoka makazi yake ya Chato, mkoani Geita.

Mkurugenzi wa Afya, Lishe na Maendeleo ya Jamii Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dk. Ntuli Kapologwe, anakiri kukua njia za asili za tiba kwa kada zote za umma, kinyume na zamani ilikuwa kwa maisha ya chini.

Mwenyekiti wa Machifu Mkoa wa Songwe, Mbeshena Nzunda, anaunga mkono akitetea miti, majani na mizizi ni msaada kwao kwa muda mrefu kutibu mafua na kikohozi, kwa kujifukiza na waliipongeza serikali kutambua na kuruhusu zitibu corona.

Kwa jumla, ilishuhudiwa tiba rasmi ya mitishamba ikileta ahueni au kuponyesha wagonjwa wa corona, kupitia mfumo wa hewa kama kifua, homa na mafua. Ni kazi iliyofanywa na 'dozi' za dawa mwarobaini, mvumbasi, mchaichai, mpera, malimao, mkaratusi, tangawizi na mimea ya kujifukiza.

**MAPYA MASOMONI**

Taaluma ya mwanafunzi inafanikishwa na njia mbili; mambo ya darasani na yasio darasani (curricular na extracurricular). Nje ya darasa kunamaanisha mambo kama michezo, usafi na gwaride.

Miezi mitatu ambayo shule zilifungwa kutokana na corona, mamlaka za kiserikali, kwa kushirikiana na wadau wengine, wakiibuka na mikakati 'maisha ya darasani yaendelee.' Hapo ukabuniwa mfumo wa elimu kuiendeshwa kupitia mtandao.

Utekelezaji na kipaumbele kiliwaangukia wanaokabiliwa na mitihani kama darasa la nne na saba kwa shule ya msingi; vidato vya pili, nne na sita kwa sekondari.

Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (UNICEF), linakadiria wanafunzi wengi kutoka nchi 188 duniani, elimu yao iliathiriwa na corona, sehemu kubwa wanatoka katika familia maskini wasio na nyenzo vifaa vya kielektroniki, radio na televisheni.

Nchini, vijana wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walibuni mbadala wakati wa corona, mtandao maalum wa 'App' uitwao 'Smart Class' kuwasaidia kusoma nyumbani, shule zilipofungwa kutokana na virusi vya corona.

Pia kuna chuo kikuu kingine kiliendesha masomo na mitihani, kwa njia ya mtandao na inaendelea kutumia hadi sasa kujihami kitaaluma.

**OFISI, TABIA & BIASHARA**

Corona ilitawanya watu katika ofisi nyingi na hata baadhi zilifungwa. Ilishuhudiwa mabadiliko ya kikazi na utamaduni mpya. Shughuli za ofisi kuendeshwa kupitia mtandao, wahusika wakiwa nyumbani na kwa walioendelea makazini, 'vigezo na masharti' ya kinga zilizingatiwa, uzoefu ukionyesha utiifu mkubwa.

Sokoni, mfano katika Manispaa ya Ilala jijini Dar es Salaam, tahadhari zilitolewa watu kuingia na kutoka kwa utaratibu maalum, huku stadi ya usafi na uzoaji taka ikiwa ya ngazi ya juu.

Elimu ya corona ilishuhudiwa kutekelezwa kwa watu kukaa umbali mita moja, kuvaa barakoa, ndoo zenye maji na kitakasa mikono juu.

Usafiri wa umma, nao ukaletewa utaratibu rasmi agizo hakuna abiria wa kusimama, katika utekezaji wake, kinyume na matarajio huenda makondakta na madereva wangekuwa wabishi, utiii ulikuwa juu.

Dar es Salaam, kulishuhudiwa uelewa hata kutotumika nguvu kwa wasimamizi wa usafiri wa umma, pia ikitoa majibu kutoripotiwa hatari za maambukizi.

Kinyume, watendaji wa daladala wakiwamo 'wapiga debe' walikuwa mstari wa mbele kufuata ushauri wa wataalamu afya, waliosisitiza abiria kunawa kabla ya kuingia katika gari, kadhalika kuvaa barakoa.

Aidha, taarifa za habari radioni, magazeti na mitandao ya kijamii zilikuwa kimbilio la wengi kutafuta mapya rasmi kuhusu corona nchini na duniani, ikiwamo darasa la mbinu mpya kukabiliana nayo.

Serikali ngazi ya juu nayo wakati huo, ilikuwa ngazi ya juu kuingilia kati wapotoshaji wa mitandao, kwa taarifa zao zisizo rasmi.

**HIFADHI YA CHAKULA**

Taharuki na aina ya maswali waliyabeba wananchi, waliohoji ikitokea amri ya serikali kama ilivyo nchi nyingine kuwaweka karantini, Je, wana akiba ya kutosha ya chakula kujimudu?

Hapo ukaibuka utamaduni mpya watu kununua chakula kingi na kuhifadhi wakijiandaa na 'dharura ya corona', japo haikutokea.

Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC), mwezi Juni mwaka jana iliwataka wananchi kuzingatia makundi muhimu ya mlo kifaya kukabili maradhi hayo.

Umma nao ukaitikia kwa kuhamia katika kula makundi matano ya vyakula vya asili: Mizizi, ndizi mbichi; pili, vyakula vya asili ya wanyama na jamii ya kunde; tatu ni mboga; nne matunda; tano sukari, mafuta na asali.

HABARI KIMATAIFA

# Tanzania yang'ara kupambana na rushwa Afrika Mashariki

**Kampala, UGANDA**

TANZANIA imetajwa kuwa kati ya nchi za Afrika Mashariki, imefanya vizuri katika kudhibiti rushwa kwenye sekta ya afya.

Zingine zilizofanya vizuri ni pamoja na nchi ya Kenya na Rwanda.

Ripoti ya Shirika la kimataifa la Transparency ya 2020, inayotolewa kila mwaka, ilibainisha hayo jana, na kwamba ilihusisha mataifa 180 na ikilenga ufisadi kwenye janga la Covid- 19.

Nchi ya Uganda katika ripoti hiyo, ilitajwa kuongoza kwa vitendo vya rushwa, kwa mujibu wa ripoti hiyo.

Ripoti inaonesha nchi za Tanzania, Kenya na Rwanda zinafanya vizuri kwenye kudhibiti rushwa na ufisadi katika sekta ya afya.

Mkurugenzi wa Shirika la Transaprency International nchini Uganda, Peter Wandera, alisema mwaka jana, shirika hilo liliangazia janga la Covid-19, kutokana na ripoti hiyo, mataifa 180 yalifanyiwa utafiti.

Alisema kwenye ripoti ilibainika mataifa mengi yalishindwa kuonesha matumizi ya fedha walizopewa kwa ajili ya vita dhidi ya virusi vya corona.

"Ripoti hii ni ya kimataifa ya masuala ya ufisadi inayotolewa na mataifa mbalimbali duniani kwa wakati mmoja kulingana na viwango vya ufisadi kila taifa na ripoti hii imezinduliwa jana, kwa wakati mmoja katika mataifa husika."

"Mwaka 2020 janga la corona limesababisha ufisadi zaidi, katika ripoti hiyo inaonesha kwamba, mataifa mengi yaliyotajwa kupanda kwa vitendo vya ufisadi imetokana na kushindwa kusimamia rasilimali za kupambana na Covid-19," alisema mkurugenzi huyo na kuongeza...

"Sasa licha ya Uganda kuonyesha jitihada katika mapambano ya kuzuia kusambaa kwa virusi vya corona, kuna tuhuma za ufisadi zinazotokana na kushindwa kuonesha matumizi halisi ya rasilimali," aliongeza Wandera. Ripoti hiyo inaonesha mwaka 2020 robo tatu ya mataifa yaliyoshiriki yalipata alama chini ya 50.

Hii inamaanisha kuwa ufisadi si katika sekta ya afya pekee, bali hata katika demokrasia ikiwa mataifa jirani na Uganda kama vile Rwanda, Tanzania na Kenya yamefanya vyema ikilinganishwa na Uganda, Rwanda ikishika nafasi ya 49, Tanzania 94, Kenya nafasi ya 124

Mamlaka nchini Uganda hazijatoa tamko lolote mpaka sasa kuhusu ripoti hiyo.

**BBC**



Watafiti wa Shirika la Afya Duniani (WHO), wakijiandaa kuelekea Wuhan, mkoa wa Hubei nchini China, jana, kwa ajili ya kuanza kufanya utafiti wa chimbuko la corona. **PICHA/AP**.

# WHO yaanza kuchunguza chimbuko la corona, China

**Wuhan, CHINA**

WATAALAMU wa afya wa Shirika la Afya Duniani (WHO), wanaochunguza chimbuko la virusi vya corona, wametembelea hospitali iliyopo mjini Wuhan, ambayo ni kati ya hospitali za kwanza kuwatibu wagonjwa wa Covid-19.

Kundi hilo linaloongozwa na WHO, lililotoka chini ya karantini ya wiki mbili, linapanga kutembelea maabara, masoko na hospitali na mjini Wuhan, ambako kisa cha kwanza cha corona kiligunduliwa mwishoni mwa mwaka 2019.

Mkuu wa Kitengo cha Dharura wa WHO, Mike Ryan, alisema kuwa shirika hilo, linatafuta uhakika na majibu kwa sasa kuhusu corona.

Mmoja wa wataalamu wa ujumbe huo wa WHO Thea Fischer, aliliambia Shirika la Habari la Reuters kwamba ni muhimu kukumbuka kuwa mafanikio ya kundi hilo na kufuatilia asili ya virusi hivyo, vinategemea kikamilifu uwezo wa kufikia vyanzo husika.

Waziri wa Idara ya Magereza nchini Uingereza, Lucy Frazer, alisema jana kuwa, nchi hiyo haitachapisha mkataba wa chanjo kati yake na kampuni ya AstraZeneca kwa sababu hatua hiyo itahatarisha usalama wa kitaifa.

Alipotakiwa na redio ya LBC kuelezea sababu ya serikali kuhofia kuhusu kuchapishwa kwa mkataba huo, Frazer alisema kuwa pale ilipostahili umma kuarifiwa kunahatarisha usalama.

Alipotakiwa kutoa ufafanuzi zaidi kuhusu suala hilo la usalama wa kitaifa, Frazer alisema kwamba huo ndio uelewa wake.

Huku hayo yakijiri, mzozo kati ya Umoja wa Ulaya (EU) na kampuni ya kutengenezea chanjo ya AstraZeneca kuhusu kutolewa kwa chanjo, kampuni hiyo ikijitetea dhidi ya madai kwamba imekiuka kujitoa kwake katika mkataba uliopo na pande hizo mbili.

Kwa mara ya kwanza, Ofisa Mkuu wa Kampuni ya AstraZeneca, Pascal Soriot, alizungumzia kuhusu mvutano huo na kukanusha madai ya EU kwamba, kampuni hiyo ilikuwa inashindwa kutimiza ahadi yake ya kutoa chanjo za virusi vya corona.

Baada ya kuchapishwa kwa mahojiano hayo, msemaji huyo, alisema kampuni hiyo ilijiondoa katika mazungumzo siku ya Jumatano kuhusu matatizo na utoaji wa chanjo.

Licha ya madai hayo kukanushwa na kampuni hiyo, ingawa saa chache baadaye, EU ilisema kuwa mazungumzo yanaendelea.

**DW**

## Wasaidizi wa rais waugua wakifungua kifurushi chenye sumu

**Tunis, TUNISIA**

WASAIDIZI wawili wa rais wa Tunisia wanaumwa baada ya kufungua kifurushi kilichofikishwa katika ofisi kikishukiwa kuwa na sumu.

Taarifa ya mkurugenzi wa ofisi ya rais ilidai, alikifungua na hakukuta barua yoyote iliyoandikwa ndani ya kifurushi hicho.

Hata hivyo baada ya kukifungua afya yake ilianza kuwa mbaya na alijihisi kama alikuwa anazimia, alikuwa na maumivu makali ya kichwa.

Mfanyakazi mwingine alikuwapo wakati wa tukio, taarifa imeeleza, alipata dalili kama hizo hali yake haikuwa mbaya.

Bahasha ilichanwa kabla ya kufikishwa kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani, taarifa iliongeza.

Haijulikani ndani ya bahasha hiyo ilikuwa na nini kilichosababisha athari kwa maofisa hao.

Taarifa hiyo ilisema vipimo vimechukuliwa na kupelekwa kwenye hospitali ya kijeshi ili kubaini sababu za maofisa kuonesha dalili hizo.

**BBC**

## Mahakama yaamuru Zuma kuchunguzwa

**Johannesburg, AFRIKA KUSINI**

MAHAKAMA ya kikatiba ya Afrika Kusini, imesema kuwa rais wa zamani Jacob Zuma ni lazima afike mbele ya jopo linalochunguza madai ya vitendo vya rushwa vilivyotokea wakati wa utawala wake.

Mahakama iliamua kuwa hakuwa na haki kukaa kimya mbele ya tume.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA SHULE

Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
IDARA YA UHAMIAJI

## OMBI LA URAIA WA TANZANIA



**BW.HERMAN SINGH NANDHRA**

Mwenye picha Juu,ni mkazi wa kata ya KICHANGANI, Mkoani Morogoro ,anaomba uraia kwa waziri wa mambo ya ndani . Nchi atokayo INDIA . Kazi yake ni Mkandarasi.Yeyote mwenye sababu kwa nini asipewe uraia atume taarifa kwa kamishina jenerali wa uhamiaji S.L.P 1181, DODOMA.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SMARTRIDE TANZANIA LIMITED** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA KLUGER** yenye namba za usajili **T 567 DSD** chasisi namba **ACU200159488** engine namba **2AZB233022** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Polisi taarifa**
**DSM/PHQ/RB/54699/2021**
**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JULIUS CHRISTOPHER SAM** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA HILUX** yenye namba za usajili **T 972 AGL** chasis namba **LN1060048248** engine namba **3L2504569** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Polisi taarifa**
**MAN/HAN/RB/51776/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**ALLY KHALIFA ALLY** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji yenye namba za usajili **MC 624 AGU** chasis namba **MD6M14PK9D4A62035** engine namba **OK4AD1066642** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Polisi taarifa**
**DAR/OST/RB/47634/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**BRYSON KIAMA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.431 CDD.**CHASSIS NAMBA **M2DDJKZZUWJ72681**. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI MBE/MBE/RB/52032/2021

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo
**KINGOLWIRA.**
Usimamizi wa mirathi No;1/2021

Ombi la **JAMILA SHOMARI MKELE,**Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **MUSSA NASSOR MGOGORO.**Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **15/02/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **14/01/2021**.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO KINGOLWIRA
MOROGORO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **WILSON KINANJA MSUYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T628 BBC.** Injini namba **QD32029347A,** Chassis namba **VWGE24044353** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi

**Taarifa ya polisi**
**ARU/ARU/RB/26203/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PAULO SAIMON PAULO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 794 DKK TOYOTA HARRIER.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.
**TAARIFA YA POLISI: DAR/OST/RB/53790/2021**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la
Nipashe kila siku

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

**HADITHI**

# HADITHI

MAUAJI ya kutisha yanatokea ndani ya gesti moja maeneo ya Kigogo jijini Dar es Salaam. Mfanyabiashara Burhan anauawa ndani ya gesti ya Tukutane, akiwa na msichana mmoja mrembo aitwaye Mwanaidi. Polisi wanawakamata watu wote waliokutwa humo, pamoja na wafanyakazi wa gesti hiyo kwa ajili ya mahojiano. Lakini inaonekana muda ambao walikuwapo wapenzi hao hakukuwa na mteja mwingine yeyote zaidi yao.

Baada ya mahojiano ya kina, inaonekana kabisa kuwa Mwanaidi ndiyo muuaji. Je, ni kweli? Kwa nini alimuua mpenzi wake wakiwa wamejifungia chumbani? Fuatilia hadithi hii kwa makini ambayo mbali na kukutia simanzi, furaha na kukuburudisha, pia itakufundisha, elimu na kufunulia mambo ambayo hukupata kuyafikiria kabla.

# Lazima Apatikane - 6

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

NI Burhan pekee ndiye alionekana kumpenda na kumuahidi akimaliza shughuli iliyomleta Dar, basi angeondoka naye kwenda mkoani Mwanza ambako sasa wangekaa na kufanya utaratibu wa kufunga ndoa mbele ya safari.

Sasa ilikuwa ni ndoto iliyoyeyuka.

Alirudi tena kuwa Mwanaidi yule yule wa kusaka wanaume ambao watampa pesa ya kula tu.

Ilikuwa ni saa 10:00 jioni wakati gari ilipomshusha nyumbani kwake Mburahati akitokea Kituo Kikuu cha Polisi.

Alilakiwa na baadhi ya majirani zake na shoga zake ambao hawakudhani kama anaweza kurudi kwa sababu anachojua kuwa ni kesi isiyo na dhamana.

Labda kama mwanaume amejifia mwenyewe gesti kwa mihemko yake, presha, au kunywa dawa za kuongeza nguvu.

Lakini mwanaume ameshindiliwa visu kifuani mara nne, si rahisi kwa polisi kumuacha mwanamke aliyekuwa ndani na mwanaume huyo.

"Pole shoga. Pole mwaya." Zilikuwa sauti za baadhi ya majirani na shoga zake ambao walishtukia tu anashuka kwenye gari.

"Ahsanteni sana." Aliwajibu, lakini akionekana hapendi sana kulizungumzia suala hilo.

"Naomba niacheni shoga zangu. Nimekaa mwezi mmoja na nusu nalala usingizi wa mang'amung'amu. Halafu halijaisha ni kwamba niko nje tu kwa dhamana." Aliwasihi shoga zake watoke nje wamuache apumzike.

Kila kitu kilichokuwa ndani kilikuwa vile vile kama siku alipoondoka kwenye kwenye gesti ya Tukutane Kigogo.

Hata hivyo kutokana na kukaa kwa muda mrefu rumande aliokaa aliona kama ndani kuna mabadiliko fulani.

Pamoja na kuachiwa, lakini bado kwenye mawazo yake alijua kabisa kuwa sakata hili bado bichi na chochote kinaweza kutokea.

********************************

Wiki moja baadaye. Mwanaidi alishaanza kuzoea maisha ya uraiani kwa mara nyingine tena. Miezi miwili aliyokaa lupango hayakuwa ya mchezo.

Alibadilisha maisha yake kwa kiasi kikubwa baada ya kurejea.




**Wiki moja baadaye. Mwanaidi alishaanza kuzoea maisha ya uraiani kwa mara nyingine tena. Miezi miwili aliyokaa lupango hayakuwa ya mchezo.**

Saluni alikokuwa anafanyia kazi aliwahi kwenda mara mbili tu. Hakuna mtu wa kutoka nyumbani mara kwa mara. Na ni mara chache sana alikuwa akikaa na jirani zako kupiga soga la hapa na pale, kama kawaida ya kinamama wa uswahilini.

Ilikuwa ni jioni moja, alipopokea mgeni ambaye hakumtambua. Cha ajabu ni kwamba mgeni yule alionekana kumtambua yeye zaidi.

Aliingia kwenye kigeti kidogo cha mabati kilichokuwa nje ya nyumba hiyo na kuongoza moja kwa moja kwenye chumba cha Mwanaidi. Akagonga mlango.

Ulifunguliwa na Mwanaidi mwenyewe. "Karibu." Alimkaribisha, lakini kwa mshangao. Ni kwamba hakuwahi kuiona sura hiyo maishani mwake.Alikuwa ni mtu wa makamu. Aliyzidi miaka 40. Mrefu mwembamba, lakini aliyeonekana kukomaa kimazoezi.

Alivaa kofia, ambayo watoto wa mjini wanaita 'kepu', iliyoziba paji la uso na sura yake usionekane vizuri.

Alivaa fulana ya kijivu ambayo ilimbana na kuonyesha kifua chake ambacho kilionekana ni mtu wa mazoezi hasa.

Alivaa suruali nyeusi na raba za bluu. "Ahsante. Nadhani wewe ndiye Mwanaidi."

Mwanaidi hakujua kama anyamaze au ajibu. Kwa sababu hakujua kama yule mtu alikuwa anajaribu kumtambua, au anamuuliza.

"Usiogope. Mimi naitwa Martin, ni rafiki yake marehemu Burhan." Alisema mtu yule ambaye alionekana kujiamini kupita kiasi na kuonekana kama anamtambua sana Mwanaidi.

"Unasemaje?" Aliuliza Mwanaidi akiwa bado amesimama mlangoni pamoja na mgeni wake.

"Ni hivi. Burhan amefariki. Lakini kuna vitu aliacha kwangu, sasa nimeona si vizuri kubaki navyo, nimtafute mtu wake wa karibu ili avichukue. Na kwa bahati nzuri alishawahi kuniambia kuwa ana mpenzi ambaye anatarajia kumuoa baadaye na akanitajia jina, ananipa picha ulizopiga nazo na hata sehemu unayofanyia kazi saluni akanitajia na hata hapa unapoishi, ndiyo maana haikuwa tabu sana kukupata." Aliyejimbulisha kwa jina la Martin alimpasha Mwanaidi.

"Vitu gani hivyo ambavyo ameviacha na kwani ni lazima nichukue mimi?"

"Hapana. Usinione hivi Mwanaidi, mimi nina pesa. Siwezi kumdhulumu marehemu vitu vyake. Alipokuwa hapa alifikia kwangu, akaishi kwangu. Sasa amekufa. Hana ndugu hapa Dar. Ndugu zake wako Mwanza. Na wamechukua mwili na kwenda kuzika bila kuuliza kitu chochote kutokana na aina ya kifo chake. Ameacha nguo zake kadhaa za gharama kubwa, viatu, pesa, kadi za benki, na vitu mbalimbali ambavyo kama ndugu yake yeyote angevipata vingemsaidia. Mimi kwa sababu alishaniambia kuhusu habari zako kuwa anakupenda sana, nimeona nikutafute ili uchukue, angalau vikusaidia kwa kipindi hiki."

Kwa mbali Mwanaidi alione anastahili kurithi vitu vya mpenzi wake Burhan, lakini kwa sababu yeye ndiye anayetuhumiwa kuua, akawa anasita kwa aibu.

"Usijali bibie. Najua ulikuwa ndani muda mrefu kwa sababu ya kesi hii, lakini hiyo haimaanishi kuwa hauna haki ya kuchukua mali zake. Na ni mimi ambazo ninazo. Twende nyumbani kwangu ukavichukue."

"Kwa nini hukuja navyo unataka niende kwako nikachukue?"

"Sikuwa na uhakika kama ninakukuta. Ndiyo maana sikuchukua."

Baada ya mazungumzo ya nusu saa. Mwanaidi alimtaka mgeni wake asubiri nje ili avae vizuri na kwenda huko kuchukua baadhi ya vitu vilivyoachwa na marehemu mpenzi wake Burhan.

Martin alikuwa amekuja na gari. Hivyo wakaingia na kuelekea maeneo ya Kawe jijini Dar es Salaam.

******************************

Gari iliingia kwenye nyumba moja ambayo ilionekana ni kama ofisi na si nyumbani kwa Martin kama alivyosema hapo mwanzo.

"Karibu, ingia ndani." Alimkaribisha.

"Shukrani", Mwanaidi alijibu.

Akajipweteka kwenye kiti kimoja kikubwa, kinene, kirefu, wakati Mwanaidi akiwa bado amesimama.

"Kaa hapo." Alimwonyesha kwenye kiti kimoja ambacho kilikuwa kinatazamana na yeye.

Mwanaidi akakaa na kutazamana uso kwa uso na Martin. Tayari uso wake ulianza kuingia mashaka.

"Nimekuchukua nyumbani kwako na kukuleta hapa kwa sababu kuna kazi moja nataka nikupe." Martin alisema huku akijitingisha kwenye kiti hicho cha kuzunguka.

"Kazi gani." Mwanaidi aliuliza kwa mshangao kwa sababu awali alivyoambiwa ni tofauti na sasa.

"Kazi ndogo tu ya mara moja."

Mwanaidi alihisi ganzi kwenye mwili wake, kwani alihisi huenda kuna kitu ambacho si cha kawaida.

Kuambiwa anakwenda kupewa vitu vya marehemu mpenzi wake na pesa zake, halafu sasa anaambiwa anataka kupewa kazi, vilimfanya kuchanganyikiwa na akanyamaza, akisubiri ni kazi gani atapewa.

"Ni kazi ya kuua mtu."

"Kuua mtu?" Mwanaidi alijikuta akiropoka kwa nguvu na kwa mshangao.

"Kwani ni kazi kubwa sana kwako? Mbona ni rahisi sana? Kwani wewe hujawahi kuua mtu?" Yalikuwa ni maswali ya Martin yalioonekana kama ya mzaha, lakini yalimtisha mno Mwanaidi kiasi cha kijasho chembamba kuanza kumtoka.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# POCHETTINO: HAIWEZEKANI KUINOA BARCA AU MADRID



**PARIS,** Ufaransa

MAURICIO Pochettino amekataa kwamba isingewezekana kwa yeye kujiunga na Klabu za LaLiga, Real Madrid au Barcelona kama kocha.

Pochettino alikuwa akihusishwa na miamba wa LaLiga hapo nyuma kabla ya kujiunga na klabu ya Ligue 1, Paris Saint-Germain mwanzoni mwa Januari.

Lakini, Pochettino amesema taarifa kwamba alipiga chini ofa hizo za kufundisha timu za Madrid na Barcelona si za kweli.

"Hii si kesi, ingawa kulikuwa na mazungumzo mengi kwa kipindi hicho," aliiambia Marca. "Tuna heshima nyingi sana katika timu hizo ambazo zimekuwa zikituvutia makocha wengi.

"Haikuwa kama hivyo ni kweli niliombwa na klabu hivyo, lakini timu ambayo ilituomba kwa dhati na upendo ilikuwa ni PSG.

Baada kuwa kocha wa Espanyol na Southampton, Pochettino aliangukia Tottenham kwa muda wa kipindi cha miaka mitano na nusu kabla ya kutimuliwa Novemba 2019.

Tayari amepata ushindi mara nne katika michezo mitano tangu achukue mikoba ya kuifundisha timu hiyo ambayo ndiyo vinara wa Ligue 1 kuelekea mchezo dhidi ya Lorient kesho, Jumapili.

# Chelsea yajitosa mazima kwa Alaba

**LONDON,** England

CHELSEA imeripotiwa kuwa "dhahiri inamtaka" David Alaba wakati mlinzi huyo makini akionekana anajiandaa kuondoka Bayern Munich kwa uhamisho huru.

Mkataba wa Alaba, mwenye umri wa miaka 28 huko Allianz Arena, unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa Juni, na kuna uwezekano mkubwa atakuwa akitafuta klabu mpya kwa kampeni ya 2021-22.

Klabu kadhaa, ikiwa ni pamoja na Manchester United, Paris Saint-Germain, Liverpool na Real Madrid, inasemekana wana nia ya kumsajili beki huyo, hivyo Chelsea hawapo peke yao katika kuiwinda saini ya staa huyo.

Wakati huo huo, ripoti ya hivi karibuni ilidai kwamba Alaba yuko mbioni kupewa mkataba mnono na Manchester City ili kuhamia Uwanja wa Etihad.

Lakini mambo yanaweza kuwa tofauti, kwa mujibu wa Sky Sports News, Chelsea pia iko katika harakati za kumsaka mchezaji huyo wa kimataifa wa Austria, ambaye amefunga mara mbili katika mechi 24 kwa mabingwa hao wa Ulaya msimu huu.

Mshindi huyo mara tisa wa Bundesliga, kwa sasa yuko huru kuingia kwenye mazungumzo na klabu za ugenini kwani ameingia miezi sita ya mwisho ya mkataba wake.





# *Nuno na mapambano ya umaskini Wolves*

**LONDON,** England

NUNO Espirito Santo, Kocha Mkuu wa Wolves alitoa kiasi cha pauni 250,000 kusaidia kupambana na umaskini katika Jiji la Wolverhampton.

Nuno, ambaye amekuwa akisimamia klabu hiyo ya Ligi Kuu tangu mwaka 2017, alitoa msaada huo kwa Wolves Foundation kuisaidia kuzindua mradi wa 'Feed Our Pack'.

Mradi huo utasaidia benki za chakula zilizochaguliwa ili kupunguza athari za umaskini wa chakula, na kusaidia wakazi walioathiriwa na janga la corona.

"Mashabiki wa Wolves na watu wa Wolverhampton wamekuwa wa kupendeza kwangu tangu nilipofika hapa karibu miaka minne iliyopita, na nilitaka kurudisha kitu na kusaidia watu ambao wanajitahidi wakati wa janga hilo," alisema Nuno akinukuliwa na BBC Sport.

"Unapoishi katika mji, unaona na kusikia jinsi watu wameathiriwa, lakini ni jiji kubwa ambalo watu wanasaidiana na kusaidiana na huu ni mradi muhimu sana kutoka kwa Wolves Foundation.

"Pamoja tuna nguvu, na ninatumahi kuwa wafuasi wetu watataka kujiunga na kuhakikisha tunawaangalia wale watu katika jamii yetu ambao wanawahitaji sana wakati huu mgumu sana."

Kuelekea kuwatembelea Crystal Palace leo Jumamosi, Wolves wako nafasi ya 13 katika jedwali la Ligi Kuu.



# KANE AIPA PIGO SPURS

**LONDON** England

NYOTA wa Tottenham na Timu ya Taifa ya England, Harry Kane, atakuwa nje ya uwanja kwa wiki kadhaa baada ya kupata majeraha.

Kane aliumia vifundo vya miguu yake yote katika mchezo wa juzi usiku dhidi ya Liverpool.

Kane amekuwa na historia ya kupata majeraha ya mara kwa mara na hali hii inamfanya awe nje ya uwanja mara nyingi. Januari 2019, Kane alikosa michezo saba kabla ya kurejea uwanjani na kisha akaumia tena Aprili 2019 ambapo alikosa michezo mingine tisa.

Msimu wa 2016/17 alikaa nje kwa wiki sita na 2017/18 alikaa nje ya uwanja kwa mwezi mmoja kwa majeraha kama hayo hayo.

Katika mchezo ambao Spurs walijikuta wakiambulia kipigo dhidi ya Liverpool, Harry Kane, aliumia baada ya kuchezewa rafu na Jordan Henderson kabla ya kugongana na Thiago Alcantara.

"Jeraha la pili lilikuwa baya zaidi ya lile la kwanza. (Kane) aliweza kuvumilia jeraha la kwanza lakini alishindwa kuvumilia yote mawili." Alisema kocha wa Spurs, Jose Mourinho.

# Gattuso: Sitaachia ngazi

**NAPLES,** Italia

GENNARO Gattuso anashangazwa na fununu juu ya hatima yake klabuni hapo, licha ya klabu kusisitiza kuwa bado ina imani naye.

Rais wa Napoli, Aurelio De Laurentiis, alitoa tamko la klabu hiyo kuwa kwa ujumla wake ipo nyuma ya kocha huyo na kumpa kila sapoti anayoihitaji.

Kwa upande wake Gattuso, yeye amesema hana haja ya kuendelea kuulizwa kama anatarajia kuacha kazi, kama ambavyo aliamua kuacha Milan. Alisema inamshtua sana anapoona watu wanamuuliza kama atajiuzulu nafasi yake.

"Niliachia nafasi yangu Milan kwa sababu sikuamini kama kulikuwa na chochote cha ziada ambacho ningeweza kufanya hapo, lakini siwezi kuachia ngazi hapa (Napoli). Niko hapa nikifanya kazi yangu," Gennaro Gattuso akinukuliwa na Sky Sport Italia.

Gattuso anasema kuwa rais aliongea na klabu na kumhakikishia juu ya hatima yake klabuni hapo, lakini kwa mtazamo wake anaona kama hakukuwa na ulazima sana kwa kuwa yeye atajitahidi kutimiza wajibu wake, na kama mchango wake hautaonekana basi hana shaka.






# *Juventus nao sasa wajitosa kwa Aouar*

**TURIN,** Italia

KLABU ya Juventus imeingia katika mbio za kumsajili kiungo Mfaransa, Houssem Aouar mwenye umri wa miaka 22, kutoka katika klabu ya Lyon.

Taarifa kutoka vyanzo mbalimbali vya michezo nchini Italia, vinasema wakala wa mchezaji huyo amefanya mazungumzo na klabu ya Juventus kuhusu uhamisho katika dirisha la majira ya joto.

Aouar amekuwa akihusishwa zaidi na timu mbalimbali ikiwamo Arsenal ya nchini Uingereza, huku mabingwa hao wa Italia wakitaka kuipokonya Gunners tonge mdomoni.

Staa huyo wa Lyon ana mkataba na miamba hao wa Ufaransa mpaka mwaka 2023 na klabu hiyo inaweza kutengeneza pesa wakimuuza katika kipindi hiki.

## HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RONALDO AINGIA MATATANI ITALIA

●●● Ni kwa kula 'bata' na mpenzi wake wakati huu ambao kuna maeneo yamezuiwa Italia...

**TURIN,** Italia

NYOTA wa Juventus, Cristiano Ronaldo, ameingia kwenye mikono ya sheria na sasa anafanyiwa uchunguzi kwa kukiuka sheria za kujilinda na mlipuko wa virusi vya corona, kwa mujibu wa Sky Sport Italia.

**Ronaldo anadaiwa kuvunja sheria hiyo baada ya kusafiri katika miji ya Piedmont na Valle d'Aosta akiwa anasherehekea siku ya kuzaliwa ya mpenzi wake, Georgina Rodriguez.**

Chapisho ambalo kwa sasa limefutwa mitandaoni, liliwaonyesha CR7 akiwa na Georgina hotelini siku ambayo mwanadada huyo alitimiza miaka 27.

Nchi ya Italia imeathirika sana na virusi vya corona huku visa vya wanaopoteza maisha kutokana na ugonjwa huo vikizidi kuripotiwa kila siku.

Mamlaka za kipolisi katika mji wa Valle d'Aosta zimethibitisha kuanza uchunguzi wa kisa hiki na endapo wawili hawa watathibitika kukiuka sheria ambayo imekataza watu kuingia maeneo yote hatarishi "orange zones", basi watachukuliwa hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kupigwa faini.

Serikali nchini Italia, imepiga marufuku watu kuingia maeneo ya hatari "orange zones" isipokuwa kwa sababu za kikazi au kwa wakazi wa eneo hilo pekee.

Ronaldo anaingia kwenye mikono ya sheria ikiwa ni mwezi tu umepita tangu alipokemewa na Waziri wa Michezo nchini humo, Vincenzo Spadafora, baada ya mchezaji huyo kusafiri kwenda Ureno kwa majukumu ya timu ya taifa muda mfupi baada ya kukutwa ameathirika na COVID-19.

## ZISIKUPITE

### KUFIKIRIA KUMUUZA MBAPPE

PARIS St-Germain itafikiria kumuuza mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe, 22, mwishoni mwa msimu huu, iwapo mshindi huyo wa Kombe la Dunia atakataa kuongeza mkataba mpya na klabu hiyo. Klabu ya Real Madrid na Liverpool zina wanawania saini yake. ***(Marca)***

### AINSLEY KUSEPA ARSENAL

MLINZI wa Arsenal na England, Ainsley Maitland-Niles, 23, yuko tayari kuondoka katika klabu hiyo kwa mkopo ili kupiga jeki nafasi yake ya kushirikishwa katika kikosi cha England cha mashindano ya Ulaya yatakayofanyika majira ya joto. ***(Mirror)***

### WEST HAM NA BRENTFORD

West Ham itabadilisha mkataba wa mkopo wa kiungo mshambuliaji wa Algeria, Said Benrahma kutoka Brentford na kumsajili kwa mkataba wa kudumu. West ham ililipa dau la pauni mlioni 4.25 kumnunua mchezaji huyo kwa mkopo na italipa dau la pauni milioni 21.75 kumnunua mchezaji huyo jumla. ***(Eurosport)***

### CHELSEA NA HAALAND, ALABA

CHELSEA ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Borrusia Dortmund, Erling Haaland, 20, pamoja na beki wa Bayern Munich raia wa Austria, David Alaba, 28, mwishoni mwa msimu huu.

### TUCHEL APOTEZEA USAJILI

KOCHA wa mpya wa Chelsea, Thomas Tuchel, hana mpango wa kuwasajili wachezaji wapya katika kipindi kilichosalia cha dirisha la uhamisho. ***(Goal)***

### AITAMANISHA ARSENAL

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amesema atafikiria uwezekano wa kuongeza muda wa mkataba wa mkopo wa Martin Odegaard ili kusalia katika klabu hiyo zaidi ya msimu huu. ***(Times)***

### LIVERPOOL KUMSAJILI GORDON

LIVERPOOL inatarajiwa kumsaini kiungo wa Derby, Kaide Gordon, 16, ambaye ameiwakilisha England katika kiwango cha juu kwenye michuano ya wachezaji wasiozidi umri wa miaka 17. ***(Goal)***

### BIESLA NA MKATABA MPYA

KOCHA wa Leeds United na Argentina, Marcelo Bielsa, 65, atasubiri hadi mwishoni mwa msimu kabla ya mazungumzo ya mkataba mpya. ***(Mirror)***

### WANOGEWA NA WILLEMS

NEWSCASTLE United ina nia ya kumsajili tena beki, Jetro Willems, 26, kuhudumu kwa mkopo katika klabu hiyo msimu uliopita kutoka klabu ya Eintracht Frankfurt. ***(Chronicle)***

### SERI KUJIUNGA FULHAM

KIUNGO wa kati wa Fulham na Ivory Coast, Jean Michael Seri, 29, anatarajiwa kujiunga na Bordeaux kwa mkopo hadi mwishoni mwa msimu. ***(Guardian)***

# Dube Chamazi leo Azam ikiivaa KMC

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Azam FC, Prince Dube, leo ataonekana kwenye Uwanja wa Azam Complex baada ya kuwa majeruhi kwa muda mrefu, timu yake itakapocheza dhidi ya KMC kwenye mechi ya kirafiki.



Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zacharia, amesema mechi hiyo itakayoanza saa 10:30 jioni ina lengo la kujiandaa na mechi za mzunguko wa pili wa Ligi Kuu, huku pia zikimpa Kocha Mkuu, George Lwandamina, nafasi ya kujua maendeleo ya kiufundi ya timu yake baada ya mazoezi yaliyoanza Jumatatu iliyopita.

Lakini ni mechi ya kwanza kwa Dube kucheza jijini Dar es Salaam, tangu alipoumia Novemba 25, mwaka jana kwenye uwanja huo huo, ilipocheza dhidi ya Yanga na kufungwa bao 1-0.

"Dube ambaye alikuwa majeruhi kwa muda mrefu amepona na anaendelea kujiimarisha kiutimamu wa mwili na kisaikolojia kwa sababu kiakili bado alikuwa akiogopa sana kujitonesha," alisema.

Dube alianza kucheza mechi za kirafiki mjini Zanzibar wakati Azam ilipobaki, baada ya kumalizika kwa michuano ya Kombe la Mapinduzi.

# Mwombeki ashinda milioni moja za Betika

**Na Mwandishi wetu**

KAMPUNI ya Michezo ya Kubahatisha ya Betika, imemtangaza Jordan Mwombeki mkazi wa Dodoma kuwa mshindi aliyejinyakulia kitita cha Sh. milioni moja katika Jackpot ya Kitonga Deile, inayofanyika kila siku.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu mshindi huyo, Mkuu wa Kitengo cha Utawala na Fedha wa kampuni hiyo, Deodata Kalumia, alisema kuwa kampuni hiyo kila siku inatoa mshindi anayejinyakulia Sh. milioni moja.

Alisema ushindi wa Mwombeki umezidi kutanua rekodi ya washindi kupitia Kitonga Deile Jackpot ambapo ameungana na washindi wengine 31 kushinda kiasi hicho cha fedha.

"Mambo yanazidi kuwa matamu kila siku mpya, na sasa mkazi wa Kanda ya Kati Dodoma, Jordan Mwombeki amejinyakulia Sh. milioni moja kwa kucheza kwa dau la Sh. 250 kupatia ubashiri, hivyo kumwezesha kujinyakulia kiasi hicho ndani ya Jackpot ya Kitonga Deile," alisema na kuongeza kuwa Betika inakutaka wewe ushinde na uzidi kuongeza idadi ya washindi wengine katika Kitonga Deile Jackpot.

# RATIBA VIPORO SIMBA, NAMUNGO YAANIKWA

**Na Mwandishi Wetu**

WAWAKILISHI pekee wa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, watashuka dimbani kucheza viporo viwili vya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Dodoma Jiji na Azam FC kabla ya kuifuata AS Vita ya DR Congo katika mechi ya awali ya hatua ya makundi ya michuano hiyo ya CAF.

Simba ambayo ni timu pekee iliyosalia kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, ipo nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 35 nyuma ya vinara Yanga yenye alama 44 baada ya michezo 18 ya mzunguko wa kwanza.

Hata hivyo, Simba ina viporo vitatu, ambavyo kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Almasi Kasongo kwenda kwa katibu mkuu wa Simba, inaeleza kuwa Simba itashuka dimbani Februari 4 na 7, mwaka huu kucheza viporo hivyo.

**"Bodi ya Ligi inakutaarifu kuwa imeipanga tarehe ya michezo minne kati ya sita iliyokuwa imeondolewa kwenye ratiba ya ligi hapo awali na sasa itachezwa Februari 4 na 7, mwaka huu kama ratiba inavyoonyesha," ilieleza.**

Kwa mujibu wa ratiba hiyo, Dodoma Jiji itaikaribisha Simba katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Februari 4, huku siku hiyo KMC FC ikiwa mwenyeji wa Namungo FC kwenye Dimba la Uhuru jijini Dar es Salaam.

Siku tatu baadaye, Februari 7, mwaka huu, Simba itashuka katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kuikaribisha Azam FC, huku Namungo ambayo inaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, siku hiyo ikiwa mwenyeji wa Ruvu Shooting katika Dimba la Majaliwa mkoani Lindi.

Simba itacheza mechi hiyo dhidi ya Azam ikiwa ni siku tano kabla ya kushuka dimbani nchini DR Congo kuvaana na AS Vita katika mechi yake ya kwanza ya hatua ya makundi ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika, CAF.

Kwa upande wa Namungo yenyewe itaivaa Ruvu Shooting ikiwa ni wiki moja kabla ya kuifuata Clube Desportivo de Agosto ya Angola kwenye mechi yao ya awali ya mchujo kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

**CHETI...**



Waziri wa Habari Utamaduni Sanaa na Michezo, Inocent Bashungwa, akimkabidhi Rais wa Shirikisho la Mpira wa Kikapu (TBF), Phares Magesa, cheti cha kuhitimu mafunzo ya Utawala Bora katika Michezo, yalioendeshwa na Chuo cha Michezo cha Malya. Hafla hiyo ilifanyika katika Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam jana, kushoto ni Mkuu wa Chuo hicho, Richard Mganga. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Bwalya asifu mtifuano Simba Super Cup*

**Na Saada Akida**

KIUNGO fundi wa Simba raia wa Zambia, Rally Bwalya, ameyasifia mashindano ya Simba Super Cup akieleza kuwa ni muhimu kwao katika kujiandaa na hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na Ligi kuu Tanzania Bara.

Simba ambayo katika hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika imepangwa kundi moja na AS Vita ya DR Congo, Al Ahly ya Misri na Al-Merrikh ya Sudan, ilianza vema mashindano hayo ya Simba Super Cup kwa kuichapa Al Hilal ya Sudan kwa mabao 4-1 kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumatano huku Bwalya akionyesha kiwango cha juu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam baada ya kumalizika kwa mechi hiyo dhidi ya Al Hilal, Bwalya alisema anafurahi kufunga bao moja na ana imani yatakuwa maandalizi mazuri kwao. Alisema kulingana na ushirikiano na umoja uliopo ndani ya kikosi hicho, ana amini inawajenga na kuwafanya kuwa imara zaidi kwa ajili ya kufikia malengo na kuwapa furaha mashabiki wao.

"Nina imani ni mashindano mazuri kwetu kwa ajili ya maandalizi kuelekea Ligi Kuu na michuano ya kimataifa kuhakikisha tunafikia malengo yanayotarajiwa na Wanasimba," alisema Bwalya.

Alisema wanakutana na timu kubwa na kupata ushindani mkubwa kwenye mashindano hayo, ambayo anaamini yamekuja muda muafaka kwao.

"Ukiangalia hizi timu ni kubwa kwa Afrika na zinashiriki Ligi ya Mabingwa Afrika, ni maandalizi mazuri kwao na kwetu, na inampa nafasi Kocha Mkuu, Didier Gomes, kuwafahamu wachezaji," alisema Bwalya.

Katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, TP Mazembe na Al Hilal zipo Kundi D pamoja na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini na CR Belouizdad ya Algeria.

# Michezo

Jumamosi Januari 30, 2021
Nipashe




Ronaldo matatani Italia

# TP MAZEMBE SASA HASIRA KWA SIMBA



Wachezaji wa TP Mazembe, wakishangili baada ya kupata bao la kuongoza kabla ya Al Hilal kutokea nyuma na kushinda 2-1 katika mechi ya Simba Super Cup, iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana. TP Mazembe itashuka tena dimbani hapo kesho kuvaana na Simba. PICHA: JUMANNE JUMA **PICHA: MTANDAO.**

## ●●● Al Hilal yazinduka yaichapa, Gomes asema ameona kitu mguuni kwa nyota wake Msimbazi, lakini...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI kesho akitarajiwa kukiongoza kikosi chake katika mechi ya pili ya michuano ya Simba Super Cup dhidi ya TP Mazembe ya DR Congo iliyoangukia kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Al Hilal ya Sudan katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jana, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, amesema amewaona wachezaji wake na kila mmoja ana kitu mguuni, hivyo anaamini muda si mrefu mambo yatanyooka.

Matokeo hayo yanaifanya sasa TP Mazembe kulazimika kupata ushindi wa kuanzia mabao 5-0 dhidi ya Simba kesho, ili kuweza kutwaa kombe hilo katika michuano hiyo ambayo ni maalum kwa ajili ya kujiandaa kwa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa timu hizo.

Lakini akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha wa Simba, Gomes alisema kwa muda mchache aliokaa na wachezaji hao amegundua kuna vitu kwa wachezaji wake na kuwataka kupambana kwa kucheza mpira wa kasi zaidi ili kuweza kupata mabao mengi katika kila mchezo.

Alisema kazi kubwa aliyonayo ni kuibadilisha timu hiyo kucheza kwa kasi na uimara wa kujilinda ili kuweza kupata matokeo mazuri ndani ya dakika 90.

"Nimeona kila kitu kwa wachezaji wangu, nina imani kila kadri ninavyowaelekeza mazoezini watazidi kuwa imara, ila kwa sasa nahitaji kuona wanacheza kwa kasi na kujilinda, huku tukitafuta idadi kubwa ya mabao katika kila mechi.

"Kazi ambayo anaifanya ni kuhakikisha wachezaji wangu wanacheza kwa kasi, jambo ambalo nalitilia mkazo kwa sababu kila mechi kwangu ni fainali kutokana na kutaka kupata ushindi ndani ya dakika 90," alisema Gomes.

Katika michuano ya Simba Super, Al Hilal jana ilizinduka na kushinda 2-1 dhidi ya TP Mazembe baada ya Wasudan hao Jumatano kubugizwa mabao 4-1 dhidi ya Simba katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Alikuwa ni mchezaji aliyetokea benchini Mohamed Mussa, aliyewanyanyua vitini mashabiki wachache wa Al Hilal waliokuwa uwanjani kwa kupachika bao dakika moja kabla ya mechi kumalizika.

Mfungaji alimzidi ujanja na kasi beki Kabaso Chongo na kuukwamisha mpira wavuni akimuacha kipa wa TP Mazembe, Sylvain Gbohouo raia wa Ivory Coast, akiruka bila mafanikio.

Dakika ya pili tu ya mchezaji Straika Mtanzania anayeichezea TP Mazembe, Thomas Ulimwengu aliingia ndani ya eneo la hatari na kupiga shuti lililopanguliwa na kipa Mohamed Al Noor na kuwa kona ambayo haikuzaa matunda.

Alikuwa ni mchezaji mpya aliyesajiliwa Septemba mwaka jana, raia wa Guinea, Moustapha Kouyate, ndiye aliyeanza kuifungia bao TP Mazembe dakika ya 11 ya mchezo, baada ya kuzuka kizaazaa kwenye lango la Al Hilal kilichotokana na kona, mpira ukagonga nguzo ya pembeni na kurejea uwanjani, kabla ya kumkuta mfungaji aliyeuweka wavuni kwa kichwa.

Ilipofika dakika ya 26, Al Hilal iliamka na kuanza kupeleka mashambulizi mfululizo kwenye lango la wapinzani wao kabla ya dakika ya 29 kusawazisha kupitia kwa straika Mkongomani, Bongonga Vinny.

## Fiston atua, akamilisha jeshi Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, sasa limekamilika kambini baada ya mshambuliaji wake mpya, Fiston Abdulrazak aliyesajiliwa katika usajili wa dirisha dogo lililofungwa Januari 15, mwaka huu kutua nchini jana.

Mshambuliaji huyo raia wa Burundi ni chaguo la Kocha Mkuu, Kaze ambaye awali alieleza anapata wakati mgumu linapokuja suala la kufanya mabadiliko kikosini kutokana na wachezaji wanaokuwa katika benchi kutokuwa na uwezo kama wanaoanza kikosi cha kwanza.

Safu ya ushambuliaji ya Yanga ilikuwa ikiongozwa na Mghana Michael Sarpong, mwenye mabao manne hadi mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Bara unamalizika akisaidiwa na Sogne Yacouba raia wa Burkina Faso.

Lakini kutua kwa Fiston ambaye kwenye michuano ya Afcon iliyopita alikuwa mmoja wa washambuliaji ambao walitupia mabao sita, huenda akaichangamsha safu ya ushambuliaji ya Yanga na kumpa uwanja mpana Kaze wa kuchagua kikosi cha kwanza.

Fiston jana alipokewa na viongozi wa Yanga wakiongozwa na Mjumbe wa Kamati ya Usajili, Injinia Hersi Said ambaye ni Mkurugenzi ndani ya Kampuni ya GSM inayoidhamini timu hiyo sambamba na baadhi ya mashabiki wa timu hiyo wakiongozwa na Ofisa Mhamasishaji, Antonio Nugaz.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

7 70856 541002 >